

# **BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**



## **TAARIFA YA UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) DARASA LA PILI 2018**

**Imeandaliwa na:  
Baraza la Mitihani la Tanzania  
S. L. P. 2624  
Dar es Salaam**

**JUNI, 2019**

# **BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**



## **TAARIFA YA UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) DARASA LA PILI, 2018**

**Imeandaliwa na:  
Baraza la Mitihani la Tanzania  
S. L. P. 2624  
Dar es Salaam**

**JUNI, 2019**

*Imechapishwa na:*

Baraza la Mitihani la Tanzania,  
S. L. P. 2624,  
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019.

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

<b>MUHTASARI MAHSUSI .....</b>	<b>vi</b>
<b>SHUKRANI .....</b>	<b>viii</b>
<b>1.0 UTANGULIZI .....</b>	<b>1</b>
<b>2.0 USAJILI NA SAMPULI YA WANAFUNZI WA STADI ZA KKK .....</b>	<b>1</b>
<b>2.1 Usajili wa Wanafunzi.....</b>	<b>1</b>
<b>2.2 Sampuli ya Upimaji .....</b>	<b>1</b>
<b>3.0 UTAYARISHAJI WA ZANA KWA AJILI YA UPIMAJI .....</b>	<b>2</b>
<b>3.1 Maandalizi ya Maswali ya Upimaji wa Stadi za KKK .....</b>	<b>3</b>
<b>3.1.1 Upangaji wa Herufi za Maswali ya Upimaji .....</b>	<b>3</b>
<b>3.1.2 Uhariri wa Maswali ya Upimaji .....</b>	<b>3</b>
<b>3.2 Utayarishaji wa Madodoso .....</b>	<b>3</b>
<b>4.0 UENDESHAJI WA SEMINA NA USIMAMIZI WA UFANYIKAJI WA UPIMAJI .....</b>	<b>4</b>
<b>4.1 Uteuzi na Semina kwa Wasimamizi .....</b>	<b>4</b>
<b>4.2 Usimamizi wa Upimaji Shuleni.....</b>	<b>4</b>
<b>5.0 USAHIHISHAJI WA UPIMAJI WA STADI ZA KKK .....</b>	<b>4</b>
<b>5.1 Washiriki wa Kazi ya Usahihishaji .....</b>	<b>4</b>
<b>5.2 Mchakato wa Kazi ya Usahihishaji .....</b>	<b>5</b>
<b>6.0 UCHAMBUZI NA MATOKEO YA UPIMAJI WA STADI ZA KKK ....</b>	<b>5</b>
<b>6.1 Viwango vya Utendaji wa Wanafunzi kwa kila Stadi za KKK.....</b>	<b>6</b>
<b>6.2 Utendaji wa Jumla katika Stadi za KKK .....</b>	<b>6</b>
<b>6.3 Viwango vya Utendaji vya Wanafunzi katika kila Stadi.....</b>	<b>7</b>
<b>6.4 Ulinganifu wa Umahiri wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi, Lugha ya Kufundishia na Shule Ilipo .....</b>	<b>9</b>
<b>6.4.1 Ulinganifu wa Umahiri wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi Katika Stadi za KKK.....</b>	<b>9</b>

<b>6.4.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi wa Shule zinazofundisha kwa lugha ya kiingereza na zinazofundisha kwa lugha ya Kiswahili .....</b>	<b>12</b>
<b>6.4.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule za Vijijini na Mijini.....</b>	<b>15</b>
<b>6.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kutoka katika Shule Zilizofanya upimaji Mara ya Kwanza 2018 na zilizorudia Upimaji mara ya Pili 2018 .....</b>	<b>17</b>
<b>6.6 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule 33 zilizofanya Upimaji mwaka 2017 na Kurudia mwaka 2018.....</b>	<b>19</b>
<b>7.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI .....</b>	<b>20</b>
<b>7.1 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Stadi ya Kusoma .....</b>	<b>21</b>
<b>7.2 Uchambuzi wa Takwimu katika Majibu ya Wanafunzi katika Stadi ya Kuandika .....</b>	<b>28</b>
<b>7.3 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Stadi ya Kuhesabu .....</b>	<b>36</b>
<b>8.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA USIMAMIZI.....</b>	<b>48</b>
<b>8.1 Taarifa za Shule kwa Ujumla .....</b>	<b>48</b>
<b>8.2 Ufundishaji wa Wanafunzi na Mafunzo kwa Walimu wa Stadi za KKK.....</b>	<b>50</b>
<b>8.3 Hali ya Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia .....</b>	<b>50</b>
<b>8.4 Miundombinu na Mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji .....</b>	<b>52</b>
<b>8.5 Mahudhurio ya Wanafunzi .....</b>	<b>53</b>
<b>9.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>54</b>
<b>9.1 Hitimisho .....</b>	<b>54</b>
<b>9.2 Mapendekezo.....</b>	<b>55</b>
<i>Kiambatisho Na. 1: Karatasi ya Upimaji Stadi ya Kusoma.....</i>	<i>57</i>
<i>Kiambatisho Na. 4: Reading Assessment Scale.....</i>	<i>74</i>
<i>Kiambatisho Na. 5: Karatasi ya Upimaji Stadi ya Kuandika.....</i>	<i>79</i>

<i>Kiambatisho Na. 6: Writing Skills.....</i>	<b>83</b>
<i>Kiambatisho Na. 7: Karatasi ya Upimaji Stadi ya Kuhesabu.....</i>	<b>87</b>
<i>Kiambatisho Na. 8: Arithmetic Skills.....</i>	<b>91</b>
<b>Kiambatisho Na. 9: Dodoso la Mwalimu Mkuu .....</b>	<b>96</b>
<b>Kiambatisho Na. 10: Dodoso la Msimamizi.....</b>	<b>100</b>

## MUHTASARI MAHSUSI

Baraza la Mitihani liliendesha upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) tarehe 11 na 12 Aprili, 2019. Upimaji ulihusisha wanafunzi waliokamilisha mtaala wa KKK Darasa la II mwaka 2018, wakati huo wakiwa wameshasoma darasa la tatu takribani miezi mitatu. Lengo la kutumia wanafunzi waliokamilisha mtaala wa KKK lilikuwa kupata tathmini ya ufanisi wa utekelezaji wa mtaala huo.

Upimaji huu ni wa tatu baada ya kufanyika upimaji wa mara ya kwanza mwaka 2015 ukifuatiwa na wa mwaka 2017. Kama ilivyokuwa mwaka 2017, upimaji wa KKK 2018 ulifanyika katika mikoa 11 ya Tanzania Bara. Upimaji wa mwaka 2018 unafanya jumla ya mikoa ambayo imeshahusishwa katika sampuli kuwa 15 ambapo kila mwaka imekuwepo angalau mikoa michache mipya.

Uchambuzi wa takwimu za wanafunzi waliofanya upimaji mwaka 2018 ulifanyika kwa kukokotoa asilimia za wanafunzi waliofanya upimaji kwa kila stadi. Ulinganifu wa umahiri ulifanyika kwa kuangalia jumla ya asilimia ya wanafunzi wenye utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana. Aidha, vigezo vilivyotumika katika ulinganifu ni jinsi, aina ya shule kwa kigezo cha lugha ya kufundishia (Kiswahili au Kiingereza) na mahali shule ilipo (Kijijini au Mjini).

Kwa ujumla, matokeo ya upimaji wa mwaka 2018 yanaonesha kuwa, umahiri wa wanafunzi katika Stadi zote tatu ni mzuri na umeongezeka ikilinganishwa na upimaji wa mwaka 2017. Katika stadi ya Kusoma asilimia 90.22 ya wanafunzi walimudu stadi hiyo ikilinganishwa na asilimia 90.13 ya wanafunzi waliomudu stadi hii mwaka 2017. Kwa upande wa Stadi ya Kuandika, asilimia 89.19 walimudu stadi hiyo ikilinganishwa na asilimia 88.86 waliomudu Kuandika mwaka 2017. Aidha, asilimia 77.49 walimudu Stadi ya Kuhesabu ikilinganishwa na asilimia 76.95 mwaka 2017.

Kama ilivyokuwa mwaka 2015 na 2017, uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, utendaji wa wanafunzi katika Stadi ya Kuhesabu umeendelea kuwa wa chini ikilinganishwa na stadi nyingine. Aidha, wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza wameendelea kuonesha utendaji mzuri zaidi ikilinganishwa na wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili. Ulinganifu wa utendaji kwa kuzingatia jinsi umeonesha kuwa, utendaji wa wasichana katika Stadi za Kusoma na Kuandika ni mzuri

zaidi kuliko wavulana wakati wavulana walikuwa na utendaji mzuri zaidi katika Stadi ya Kuhesabu. Uchambuzi zaidi umeonesha kuwa shule zilizoko mijini zilikuwa na utendaji mzuri zaidi kuliko shule zilizopo vijijini katika stadi zote.

Uchambuzi wa madodoso ulionesha kuwa, asilimia 98.33 ya shule zilizofanyiwa upimaji zilikuwa na vitabu vya kiada vinavyotumika kufundishia KKK, vitabu vya ziada kwa ajili ya mazoezi ya Stadi za Kuhesabu na vifaa. Kwa ujumla takwimu zinaonesha kupungua kwa changamoto ya uhaba wa vitabu vya kufundishia stadi za KKK ikilinganishwa na taarifa kuhusu uwepo wa vifaa hivyo katika upimaji wa KKK 2017. Kwa upande wa mahudhurio, kiwango cha utoro kimepungua toka asilimia 86.5 katika upimaji wa 2017 hadi asilimia 68.6 katika upimaji wa mwaka 2018, jambo linaloonesha kuwa juhudi za makusudi zilifanyika za uwepo wa wanafunzi shuleni.

Kutokana na matokeo ya upimaji wa KKK 2018, Baraza la mitihani linashauri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia taasisi na mamlaka zake kufanya ufuatiliaji zaidi kwenye ufundishaji na ujifunzaji ili kuinua kiwango cha ujifunzaji na ufundishaji wa Stadi ya Kuhesabu ambayo utendaji wake umeendelea kuwa wa chini ikilinganishwa na Stadi za Kusoma na Kuandika. Ufuatiliaji pia ufanyike ili kuondoa tofauti ya kiutendaji inayojitokeza kati ya wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika kujifunza kwa upande mmoja, na walioko mijini na vijijini kwa upande mwingine. Aidha, Baraza linashauri Maafisa Elimu wa Mikoja na Halmshauri zote nchini waendeleo kutafuta ufumbuzi wa tatizo la utoro ambalo bado linaonekana kuwa changamoto katika mahudhurio ya wanafunzi.



Dkt. Charles E. Msonde  
**KATIBU MTENDAJI**



## **SHUKRANI**

Upimaji wa stadi za KKK mwaka 2018 ulifanikiwa kwa jitihada za wadau mbalimbali wa Elimu. Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika kufanikisha kazi ya upimaji huo.

Kipekee, Baraza la Mitihani linatoa shukrani kwa wafanyakazi wake walioshiriki kufanya maandalizi ya zana za upimaji, ufuatiliaji wa ufanyikaji wa upimaji na kusimamia usahihihaji wa skripti za wanafunzi. Pia, kwa kufanya uchambuzi wa madodoso, matokeo ya upimaji na uandishi wa taarifa hii.

Baraza la Mitihani pia linatoa shukrani za dhati kwa viongozi wa Elimu ngazi ya Mkoa na Wilaya zilizohusishwa katika upimaji huu kwa kuhakikisha upimaji unafanyika kikamilifu. Aidha, Baraza la Mitihani linatoa shukrani kwa Walimu wa Shule za Msingi waliofanya kazi ya kusimamia na kusahihihisha. Baraza linawashukuru pia wanafunzi wote wa shule za msingi waliofanya upimaji huu.



## **1.0 UTANGULIZI**

Upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) una lengo la kufanya tathmini ya maendeleo ya wanafunzi katika stadi husika na uelewa wa umahiri wa stadi hizo.

Taarifa hii inaelezea kuhusu uendeshaji wa upimaji wa stadi za KKK kwa kubainisha sampuli na usajili wa wanafunzi, utayarishaji wa zana za upimaji na namna usimamizi ulivyofanyika. Pia taarifa inaelezea kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa vitendea kazi (teaching and learning materials) na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji shuleni. Aidha, taarifa inafafanua jinsi zoezi la usahihishaji na uchambuzi wa matokeo ya wanafunzi ulivyofanyika. Hitimisho pamoja na mapendekezo vimetolewa mwishoni mwa taarifa hii.

## **2.0 USAJILI NA SAMPULI YA WANAFUNZI WA STADI ZA KKK**

Hatua ya kwanza ya mchakato wa upimaji wa stadi za KKK ulikuwa ni kubainisha sampuli ya wanafunzi wa kufanyiwa upimaji. Mfumo wa usajili wa Baraza la Mitihani la Tanzania (PReM) ulitumika katika kubainisha sampuli hiyo. Sampuli ilibainisha mikoa, halmashauri na shule zilizochaguliwa kufanya upimaji.

### **2.1 Usajili wa Wanafunzi**

Taarifa za wanafunzi zilichukuliwa katika mfumo wa usajili wa wanafunzi wa Baraza la Mitihani (PReM) baada ya kila shule kufanya usajili wa wanafunzi wake. Aidha, nyaraka za usajili kama vile *Collective Attendance List* (CAL) na *Individual Subject Attendance List* (ISAL) ziliandaliwa ili zitumike wakati wa upimaji. ISAL ilitumika kurekodi mahudhurio katika Stadi ya Kusoma pekee na CAL ilitumika kwa Stadi zote tatu.

Taarifa za usajili zinaonesha kuwa, jumla ya wanafunzi 6,941 kutoka shule 66 zilizoteuliwa katika sampuli walisajiliwa kufanya upimaji mwaka 2018.

### **2.2 Sampuli ya Upimaji**

Uteuzi wa shule zilizohusika katika upimaji ulizingatia Kanda za Kielimu. Utaratibu wa kupata sampuli lengwa (purposive sampling) ulitumika kuteua sampuli ya Kanda ambapo Kanda zote 11 zilihusishwa. Kila Kanda iliwakilishwa na mkoa mmoja

uliochaguliwa kwa njia ya sampuli nasibu (random sampling). Aidha, halmashauri mbili kutoka mikoa husika zilichaguliwa kwa njia ya bahati nasibu, hivyo kufanya jumla ya halmashauri zilizohusika katika upimaji kuwa 22.

Uchaguzi wa sampuli za shule katika halmashauri ulifanyika kwa kutumia uteuzi kimatabaka (stratified random sampling) ambapo katika kila halmashauri ziliteuliwa shule tatu, hivyo kufanya jumla ya shule kuwa 66. Vigezo vilivyozingatiwa katika uteuzi wa sampuli ya shule ni ufaulu, mahali shule ilipo (Kijijini au Mjini) na lugha ya kufundishia (Kiingereza au Kiswahili). Katika shule zilizoteuliwa, mbili zinatumia mfumo wa lugha ya Kiswahili na moja inatumia lugha ya Kiingereza. Jedwali Na. 1 linaonesha mtawanyiko wa uteuzi wa sampuli.

**Jedwali Na 1: Mtawanyiko wa Sampuli ya Upimaji KKK 2018**

Na	Kanda	Mkoa	Halmashauri
1.	Dar es Salaam	Dar es Salaam	Temeke, Ubungo
2.	Kaskazini Mashariki	Kilimanjaro	Hai, Moshi (V)
3.	Mashariki	Morogoro	Morogoro (M), Mvomero
4.	Kaskazini Magharibi	Arusha	Arusha (M), Monduli
5.	Ziwa Magharibi	Kagera	Bukoba (M), Bukoba (V)
6.	Ziwa	Mwanza	Magu, Mwanza (J)
7.	Nyanda za Juu	Mbeya	Mbeya (J), Mbeya (V)
8.	Nyanda za Juu Kusini	Njombe	Njombe (M), Wanging'ombe
9.	Kusini	Mtwara	Mtwara (M), Mtwara (V)
10.	Kati	Singida	Singida (M), Singida (V)
11.	Magharibi	Tabora	Nzega (M), Tabora (M)

### 3.0 UTAYARISHAJI WA ZANA KWA AJILI YA UPIMAJI

Katika kufanikisha upimaji wa stadi za KKK, zana za upimaji ambazo ni maswali ya upimaji wa kila stadi na madodoso ziliandaliwa.

### **3.1 Maandalizi ya Maswali ya Upimaji wa Stadi za KKK**

Karatasi za upimaji ziliandaliwa na zilifanyiwa uhariri na wataalam sita (06) wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania kwa kufuata taratibu na miongozo ya Baraza la Mitihani.

#### **3.1.1 Upangaji wa Herufi za Maswali ya Upimaji**

Uhariri na upangaji herufi (Typesetting) ulifanywa na Maafisa Mitihani wa Baraza la Mitihani la Tanzania ambao ni wataalam wa masomo husika (Kiambatanisho 1 – 8). Maswali hayo yaliandaliwa kwa kuzingatia vigezo vya utendaji vilivyoainishwa katika muhtasari wa mwaka 2015 ambavyo ni; utendaji hafifu, utendaji wa wastani, utendaji mzuri na utendaji mzuri sana. Maswali ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho yalichapwa kwa kutumia maandishi ya Nukta Nundu.

#### **3.1.2 Uhariri wa Maswali ya Upimaji**

Uhariri wa mwisho wa maswali ya upimaji ulifanywa na Mkuu wa Idara ya Usanifu na Ukuzaji wa Mitihani na Naibu Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania. Dosari zilizobainishwa na wahariri zilifanyiwa marekebisho na Maafisa Mitihani husika.

### **3.2 Utayarishaji wa Madodoso**

Upimaji wa Stadi za KKK uliambatana na madodoso (Kiambatanisho 9-10) ambayo yalitakiwa kujazwa na Walimu Wakuu na Wasimamizi. Madodoso hayo yalitumika kukusanya taarifa mbalimbali kuhusu upimaji wa stadi za KKK. Madodoso yaliyojazwa na Wasimamizi yalilenga kukusanya taarifa kuhusu mazingira ya ufanyikaji wa upimaji wakati madodoso yaliyojazwa na Walimu Wakuu yalilenga kukusanya taarifa kuhusu shule kwa ujumla pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Pia yalikusanya taarifa za mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji na taarifa nyinginezo zilizohusu stadi za KKK.

## **4.0 UENDESHAJI WA SEMINA NA USIMAMIZI WA UFANYIKAJI WA UPIMAJI**

### **4.1 Uteuzi na Semina kwa Wasimamizi**

Ili kuhakikisha kazi ya usimamizi inakuwa na ufanisi, wasimamizi waliteuliwa na kupatiwa semina ya namna ya kusimamia upimaji. Baraza la Mitihani liliendesha semina kwa maafisa mitihani 66 ili kuwapa ujuzi wa kuendesha semina kwa wasimamizi wa kila shule. Semina iliyotolewa kwa maafisa wa Baraza ilifanyika katika ukumbi wa mikutano wa Baraza la Mitihani chini ya usimamizi wa Menejimenti ya Baraza. Wasimamizi wa kila shule walipewa semina na Maafisa wa Baraza la Mitihani la Tanzania ambao walikuwa wamepewa semina ya kuwawezesha kuendesha semina hizo katika vituo vya usimamizi.

Semina kwa wasimamizi ilifanyika katika shule husika kwa siku moja, tarehe 10/04/2019. Washiriki wa Semina hiyo walikuwa walimu 696 wanaofundisha katika shule zilizoteuliwa katika sampuli ya upimaji.

### **4.2 Usimamizi wa Upimaji Shuleni**

Upimaji ulifanyika kwa siku mbili, tarehe 11/04/2019 na 12/04/2019 katika vituo 66 vilivyokuwa vimeteuliwa. Kila kituo cha upimaji kilikuwa na Msimamizi Mkuu ambaye ni Afisa mitihani wa Baraza la Mitihani na wasimamizi wa vyumba. Wasimamizi wote walikuwa ni walimu wanaofundisha katika shule/kituo husika. Kila msimamizi alisimamia wanafunzi ishirini na tano (25) katika upimaji wa Kuandika na Kuhesabu. Katika upimaji wa stadi ya Kusoma, msimamizi mmoja alisimamia wanafunzi wapatao kumi (10). Aidha, kila kituo kilikuwa na Afisa mmoja wa Baraza la Mitihani ambaye baada ya kutoa mafunzo kwa wasimamizi, alifanya kazi ya ufuatiliaji wa ufanyikaji wa upimaji.

## **5.0 USAHIHISHAJI WA UPIMAJI WA STADI ZA KKK**

### **5.1 Washiriki wa Kazi ya Usahihishaji**

Kazi ya usahihishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu 2018 ilihusisha jumla ya washiriki 93 kati ya 97 waliotarajiwa, sawa na asilimia 95.8 ya walioalikwa. Washiriki hao walikuwa

walimu wa shule za msingi, walimu wa shule za sekondari, wataalamu wa maandishi ya wasioona na wafanyakazi wa NECTA. Jedwali Na.2 linaonesha mchanganuo wa washiriki.

## Jedwali Na. 2: Washiriki wa Usahihishaji

Na.	Aina ya Washiriki	Idadi
1.	Wafanyakazi wa Baraza la Mitihani	23
2.	Wasahihishaji (Walimu)	56
3.	Wahahakiki na Waingizaji wa Alama	9
4.	Daktari na Muuguzi	2
5.	Maafisa Elimu Taaluma (W)	2
6.	Mwakilishi TAMISEMI	1
	<b>Jumla</b>	<b>93</b>

### 5.2 Mchakato wa Kazi ya Usahihishaji

Usahihishaji wa skripti za stadi ya Kuandika na Kuhesabu ulifanyika kwa kutumia mfumo wa 'Conveyor Belt'.<sup>1</sup> Skripti za watahiniwa wasioona kwa stadi za Kuandika na Kuhesabu zilibadilishwa na kuwa katika maandishi ya kawaida kabla ya kusahihishwa. Baada ya usahihishaji, skripti zilihakikiwa na alama ziliingizwa kwenye kompyuta. Karatasi za Skeli za Upimaji wa Stadi ya Kusoma zilizotumika kurekodi alama za wanafunzi katika upimaji wa stadi hiyo shuleni zilihakikiwa na alama ziliingizwa kwenye kompyuta. Aidha, Skeli za Upimaji za wanafunzi wasioona kwa Stadi ya Kusoma ziliwekwa alama na wasimamizi vituoni kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wanaoona. Waingizaji na wahakiki wa alama walikuwa walimu kutoka shule za sekondari wenye ujuzi na uzoefu wa kompyuta.

### 6.0 UCHAMBUZI NA MATOKEO YA UPIMAJI WA STADI ZA KKK

Kati ya wanafunzi 7,034 waliosajiliwa, 5,771 (82.04%) walifanya upimaji. Hivyo, jumla ya wanafunzi 1,263 wakiwemo wavulana 734 na wasichana 529 sawa na asilimia 17.96 hawakufanya upimaji. Changamoto zilizosababisha wanafunzi kutohudhuria katika upimaji ni pamoja na utoro, kuhama, kukariri darasa, ugonjwa na kufariki.

<sup>1</sup> Conveyor belt ni mtindo wa usahihishaji ambapo msahihishaji mmoja husahihisha swali moja katika skripti na kumpatia msahihishaji mwingine kusahihisha swali lingine hadi inapofika kwa mwingizaji alama.

## 6.1 Viwango vya Utendaji wa Wanafunzi kwa kila Stadi za KKK

Katika kufanya uchambuzi wa matokeo kwa ujumla na katika kila stadi, viwango vya utendaji vimepangwa katika makundi manne ambayo ni: utendaji hafifu, utendaji wa wastani, utendaji mzuri na utendaji mzuri sana.

Karatasi ya upimaji katika kila stadi ilikuwa na jumla ya alama 50, hivyo utendaji wa mwanafunzi ulipangwa kwa kuzingatia jumla ya alama walizopata wanafunzi. Mwanafunzi alihesabika kuwa na utendaji **mzuri sana** kama aliweza kupata alama 39 hadi 50. Mwanafunzi aliyepata alama 26 hadi 38 alihesabika kuwa na utendaji **mzuri**. Kwa upande mwingine, mwanafunzi aliyepata alama 13 hadi 25 alikuwa na utendaji wa **wastani** na mwanafunzi aliyepata alama 0 hadi 12 alikuwa na utendaji **hafifu**. Wanafunzi walihesabika kuwa walifanya vizuri endapo walipata alama 13 hadi 50 ambazo zinawakilisha madaraja ya viwango vya utendaji wa **wastani** hadi **mzuri sana**.

## 6.2 Utendaji wa Jumla katika Stadi za KKK

Takwimu za jumla za matokeo zinaonesha kuwa, viwango vya utendaji vilivyofikiwa na wanafunzi waliofanya upimaji katika stadi zote (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu) ni vizuri. Takwimu hizo zimeoneshwa katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Utendaji wa Jumla wa Wanafunzi katika Stadi za KKK**

Na	Stadi	Waliofanya	Utendaji (Wastani hadi Mzuri sana)	(%)
1.	Kusoma	5,621	5,071	90.22
2.	Kuandika	5,677	5,063	89.18
3.	Kuhesabu	5,682	4,403	77.49

Uchambuzi wa takwimu katika Jedwali Na. 3 unaonesha kuwa, wanafunzi 5,621 walifanya Stadi ya Kusoma. Kati yao wanafunzi 5,071 sawa na asilimia 90.22 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Wanafunzi waliofanya Stadi ya Kuandika walikuwa 5,677 ambapo wanafunzi 5,063 sawa na asilimia 89.18



walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Kwa upande wa Stadi ya Kuhesabu, wanafunzi 5,682 walifanya upimaji ambapo wanafunzi 4,403 sawa na asilimia 77.49 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Hivyo, matokeo ya jumla yanaonesha kuwa, asilimia 96.01 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana ambao unawawezesha kumudu masomo ya ngazi inayofuata.

Katika matokeo hayo ya upimaji wa mwaka 2018 kulikuwa na ongezeko dogo la wanafunzi wenye umahiri wa wastani hadi mzuri sana katika kila stadi ikilinganishwa na upimaji wa mwaka 2017. Kwa mfano, katika Stadi ya Kusoma, wanafunzi wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana wamekuwa na ongezeko la asilimia 0.09 kutoka asilimia 90.13 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 90.22 mwaka 2018. Vivyo hivyo, katika Stadi ya Kuandika, wanafunzi wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana waliongezeka kutoka asilimia 88.86 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 89.18 mwaka 2018, yaani ongezeko la asilimia 0.32.

Kwa upande wa Stadi ya Kuhesabu, wanafunzi wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana wameongezeka kutoka asilimia 76.95 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 77.49 mwaka 2018. Hata hivyo, bado tatizo la wanafunzi kutokuwa na utendaji mzuri katika Stadi ya Kuhesabu limeendelea kujitokeza kwani stadi hiyo ina asilimia kubwa zaidi (22.54%) ya wanafunzi wenye utendaji hafifu ikifuatiwa na Stadi ya Kuandika (10.82%). Wanafunzi wengi wameonekana kuwa na utendaji mzuri zaidi katika Stadi ya Kusoma ambapo wanafunzi wenye utendaji hafifu ni asilimia 9.78.

Ongezeko la wanafunzi wenye umahiri wa wastani hadi mzuri sana linaonesha kuwa, juhudi za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika shule za msingi zinaendelea kuchukuliwa na kuleta mafanikio.

### **6.3 Viwango vya Utendaji vya Wanafunzi katika kila Stadi**

Uchambuzi ulifanyika katika kila stadi kwa lengo la kuona mtawanyiko wa wanafunzi katika viwango vya utendaji. Kwa

kuzingatia viwango hivyo, utendaji wa wanafunzi kwa kila stadi vimewasilishwa katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4: Mtawanyiko wa Wanafunzi katika kila Kiwango cha Utendaji**

Stadi	Walio pimwa	Hafifu		Wastani		Mzuri		Mzuri Sana	
		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
Kusoma	5,621	550	9.78	216	3.84	469	8.35	4,386	78.03
Kuandika	5,677	614	10.82	857	15.10	1,891	33.31	2,315	40.78
Kuhesabu	5,682	1,279	22.51	1300	22.88	1,967	34.62	1,136	19.99

Takwimu katika Jedwali Na. 4 zinaonesha kuwa, kwa ujumla asilimia ya wanafunzi wenye viwango hafifu vya utendaji katika stadi zote imepungua ingawa ni kwa kiwango kidogo. Kwa mfano, katika Stadi ya Kusoma, asilimia ya wanafunzi wenye utendaji wa wastani na utendaji mzuri imepungua na kusababisha ongezeko la asilimia 12.70 ya wanafunzi wenye utendaji mzuri sana. Utendaji mzuri sana umefikia asilimia 78.03 ikilinganishwa na asilimia 65.33 ya wanafunzi wenye utendaji kama huo katika upimaji wa mwaka 2017.

Katika Stadi ya Kuandika, takwimu zinaonesha kushuka kwa asilimia ya wanafunzi wenye kiwango cha utendaji mzuri sana kwa asilimia 9.46, yaani kutoka asilimia 50.23 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 40.78 katika upimaji wa mwaka 2018. Pamoja na kupungua kwa wanafunzi wenye utendaji mzuri sana katika Stadi ya Kuandika kuna ongezeko la wanafunzi wenye utendaji wa wastani na utendaji mzuri kutoka asilimia 12.13 na 26.50 mwaka 2017 hadi asilimia 15.10 na 33.32 mwaka 2018 mtawalia.

Katika Stadi ya Kuhesabu, asilimia ya wanafunzi wenye utendaji hafifu imepungua kwa asilimia 0.49 kutoka asilimia 23 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 22.51 katika upimaji wa mwaka 2018 jambo linaloonesha kuwa kuna badiliko chanya.

Hata hivyo, pamoja na badiliko hilo asilimia ya wanafunzi wenye utendaji mzuri sana nayo imepungua kwa kiwango cha asilimia 0.25 kutoka asilimia 20.24 mwaka 2017 hadi asilimia 19.99 mwaka 2018. Vilevile, wanafunzi wenye kiwango cha utendaji mzuri wamepungua kwa asilimia 0.36 kutoka asilimia 34.98 mwaka 2017 hadi 34.62 mwaka 2018. Hivyo, ongezeko limejitokeza kwa wanafunzi wenye utendaji wa wastani kwa asilimia 1.01 kutoka asilimia 21.87 mwaka 2017 hadi asilimia 22.88 mwaka 2018.


Kupungua kwa wanafunzi wenye utendaji hafifu katika Stadi ya Kuhesabu na kuongezeka kwa asilimia ya wanafunzi katika kiwango cha utendaji wa wastani ni ishara ya kuimarika kwa ujifunzaji katika stadi hii.

#### **6.4 Ulinganifu wa Umahiri wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi, Lugha ya Kufundishia na Shule Ilipo**

Uchambuzi ulifanyika kwa kufanya ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kutokana na jinsi, lugha ya kufundishia na kujifunzia na mahali shule ilipo (mjini au kijijini) ili kubaini kama kuna tofauti katika utendaji na sababu za tofauti hizo.

##### **6.4.1 Ulinganifu wa Umahiri wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi Katika Stadi za KKK**

Uchambuzi wa takwimu ulifanyika kwa kuzingatia jinsi ili kuona utendaji wa wanafunzi katika makundi haya mawili. Takwimu zinaonesha kuwa, wasichana wana utendaji wa juu zaidi ikilinganishwa na wavulana. Chati Na. 1 inaonesha utendaji kijinsi kwa Stadi ya Kusoma na Kuandika.



**Chati Na. 1:** Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia jinsi katika Stadi za Kusoma na Kuandika.


Takwimu katika Chati Na. 1 zinaonesha kuwa wasichana walikuwa na utendaji mzuri zaidi katika Stadi ya Kusoma na Kuandika. Matokeo hayo yanashabihiana na yale ya upimaji wa mwaka 2017 ambapo katika Stadi ya Kusoma na Kuandika, wasichana walionesha utendaji mzuri zaidi katika vipengele vyote vya stadi hizo ikilinganishwa na wavulana.

Upimaji wa mwaka 2018 pia takwimu zinaonesha kuwa, wasichana walikuwa na asilimia 91.60 ya umahiri kwenye swali la 1 lililohusu kusoma maneno ikilinganishwa na asilimia 88.19 ya wavulana kwenye umahiri huo. Wasichana pia walikuwa na utendaji mzuri zaidi katika umahiri mahsusi wa kusoma sentensi kwenye swali la 2 ambapo wasichana wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana walikuwa asilimia 92.05 ikilinganishwa na asilimia 88.48 ya wavulana wenye utendaji kama huo. Mwelekeo huo ulijitokeza pia katika kusoma kifungu cha maneno na kisha kujibu maswali kwenye swali la 3 ambapo wasichana wenye utendaji wa wastani hadi

mzuri sana walikuwa asilimia 85.30 ikilinganishwa na asilimia 79.55 ya wavulana wenye utendaji kama huo.

Katika stadi ya kuandika, wasichana pia walikuwa na utendaji wa juu kuliko wavulana katika umahiri mahsusi uliopimwa ambapo, katika stadi ya kuandika maneno (majina), wasichana wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana walikuwa asilimia 91.37 ikilinganishwa na asilimia 87.04 ya wavulana wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Katika swali la 2 lililopima umahiri mahsusi wa kutambua herufi kubwa na ndogo, wasichana wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana walikuwa asilimia 77.04 ikilinganishwa na asilimia 76.31 ya wavulana wenye utendaji kama huo. Katika umahiri wa kunakili kifungu cha habari na matumizi ya alama za uandishi, wasichana wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana walikuwa asilimia 81.65 ikilinganishwa na asilimia 75.71 ya wavulana wenye utendaji huo. Utendaji wa wanafunzi katika Stadi za Kuandika na Kusoma mwaka 2018 unaonesha kushabihiana na ule wa mwaka 2017 ambapo wasichana walifanya vizuri zaidi kuliko wavulana.

Tofauti ya utendaji wa wanafunzi katika Stadi ya Kuhesabu kati ya wavulana na wasichana haikuwa bayana. Hata hivyo, wasichana walionesha utendaji mzuri zaidi katika umahiri mahususi uliopimwa isipokuwa katika dhana ya namba ambapo wavulana walikuwa na utendaji mzuri zaidi kuliko wasichana. Chati Na. 2 inaonesha utendaji wa wasichana na wavulana katika Stadi ya Kuhesabu.



**Chati Na. 2:** Utendaji wa wavulana na wasichana katika Stadi ya Kuhesabu.

Takwimu katika Chati Na. 2 zinaonesha kuwa, utendaji wa wavulana katika dhana ya namba ulikuwa asilimia 64.10 ikilinganishwa na asilimia 62.07 ya wasichana wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Kwa upande wa dhana ya kujumlisha, dhana ya kutoa na kufumbua mafumbo, wasichana walikuwa na utendaji mzuri zaidi ikilinganishwa na wavulana ingawa tofauti ni ndogo ambapo wasichana wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana walikuwa asilimia 68.53, 54.49 na 44.60 ikilinganishwa na asilimia 68.18, 52.39 na 44.31 za wavulana mtawalia.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa, viwango vya utendaji wa wasichana na wavulana katika stadi zote vinatofautiana kidogo. Jambo hilo linaonesha kuwa, jinsi ya mwanafunzi haina athari katika ufundishaji na ujifunzaji endapo wote watapewa fursa sawa na mazingira rafiki wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

#### **6.4.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi wa Shule zinazofundisha kwa lugha ya Kiingereza na zinazofundisha kwa lugha ya Kiswahili**

Uchambuzi wa takwimu ulifanyika ili kufanya ulinganifu wa umahiri wa wanafunzi katika shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiingereza na zile zinazotumia lugha ya Kiswahili.


Ulinganifu huo ulifanyika kwa kuangalia jumla ya asilimia ya wanafunzi wenye utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana katika kila stadi na kisha kulinganisha takwimu za makundi hayo mawili.

Uchambuzi wa takwimu ulionesha kuwa, wanafunzi wanaosoma katika shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiingereza walikuwa na utendaji mzuri zaidi ikilinganishwa na wanafunzi wanaosoma katika shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiswahili katika stadi zote. Hata hivyo, tofauti hiyo haikuweza kuhusishwa na lugha ya kufundishia kutokana na ukweli kuwa Kiswahili ndiyo lugha inayotumiwa na Watanzania wengi na imeenea hadi vijijini.

Takwimu zinaonesha kuwa, katika Stadi ya Kusoma, wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza walifanya vizuri zaidi kwa asilimia 9.50 ikilinganishwa na wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili. Hii inatokana na asilimia 98.16 ya wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana ikilinganishwa na asilimia 88.66 ya wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili wenye utendaji kama huo.

Katika Stadi ya Kuandika, makundi haya mawili yalitofautiana kwa asilimia 8.51. Tofauti hiyo inatokana na wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana wa asilimia 96.31 wakati shule zinazotumia lugha ya Kiswahili walikuwa asilimia 87.80.

Kwa upande wa Stadi ya Kuhesabu, tofauti ya utendaji kati ya wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili na wanaotumia lugha ya Kiingereza ilikuwa kubwa zaidi (24.96%) ikilinganishwa na tofauti iliyopo kwenye Stadi za Kusoma na Kuandika. Katika Stadi ya Kuhesabu, asilimia 98.37 ya wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana ikilinganishwa na shule zinazotumia lugha ya Kiswahili (73.41%) kama inavyoonekana katika Chatii Na. 3.



**Chati Na. 3:** Utendaji wa Wanafunzi katika Shule Zinazofundisha kwa Lugha ya Kiswahili na Zinazofundisha kwa Lugha ya Kiingereza

Chati Na. 3 inaonesha kuwa wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza wana utendaji mzuri zaidi katika stadi zote na kwamba tofauti ni kubwa zaidi katika Stadi ya Kuhesabu.

Tofauti kati ya wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiswahili na wanaotumia lugha ya Kiingereza ilianza kujitokeza katika matokeo ya upimaji wa stadi za KKK mwaka 2015 na 2017. Ili kubaini sababu za kutofautiana, dodoso lilitumika kupata taarifa ya mazingira na hali ya ufundishaji na ujifunzaji shuleni.

Pamoja na mambo mengine, dodoso liliuliza vifaa vya kufundishia kama vile vitabu vya kiada na ziada, idadi ya mikondo na walimu wanaofundisha KKK kwa nia ya kuona kama uwiano kati ya wanafunzi na walimu katika ngazi hiyo unazingatiwa. Upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada pamoja na uwepo wa vyumba vya kufundishia na kujifunzia uliripotiwa kuwa mzuri kwa shule zote za



English Media na Kiswahili Media. Tofauti ilijitokeza katika uwiano kati ya walimu na wanafunzi.

Kwa upande wa uwiano wa walimu na wanafunzi, asilimia 63.60 ya shule zilizohusika katika upimaji zina uwiano wa 1:40 (mwalimu mmoja kwa wanafunzi 40). Uwiano huu ndio ulioelekezwa kwenye Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2007. Hii inamaanisha kuwa, asilimia 36.40 ya shule zina wanafunzi wanaozidi uwiano wa 1:40 kama ulivyoainishwa kwenye mtaala. Matokeo haya yalitarajiwa kwa kuwa udahili wa wanafunzi umeongezeka, ikiwa ni moja ya changamoto chanya ya matokeo ya serikali ya kuondoa ada kwa wanafunzi wa elimu msingi. Kutokana na ukweli huu, shule 16 sawa na asilimia 24.24 zilikuwa na wanafunzi zaidi ya 70 kwa mkondo mmoja.

Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa, karibu shule zote zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia zinakidhi matakwa ya mtaala. Ni shule moja tu ya aina hii sawa na asilimia 1.5 ambayo ilikuwa imezidi uwiano ulioelekezwa.

Hivyo, tofauti za utendaji kwa wanafunzi wanaosoma katika shule za English na Kiswahili media inaweza kuwa inasababishwa na changamoto ya uwiano wa walimu na wanafunzi, kwani wanafunzi wanaosoma stadi za KKK wanahitaji ufuatiliaji wa karibu ikiwemo ufuatiliaji wa maendeleo ya tabia zao.

#### **6.4.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule za Vijijini na Mijini**

Uchambuzi ulifanyika kwa lengo la kubaini tofauti za utendaji wa wanafunzi katika stadi za KKK kati ya shule za vijijini na mijini. Ulinganifu ulifanyika kwa kuangalia jumla ya asilimia ya wanafunzi wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Takwimu zinaonesha kuwa, katika upimaji wa mwaka 2018 wanafunzi waliopo katika shule zilizoko mijini wameonekana kuwa na utendaji mzuri zaidi katika stadi zote ikilinganishwa na wanafunzi waliopo katika shule za vijijini.


Uchambuzi pia umeonesha kuwa, katika upimaji wa mwaka 2018, utendaji wa wanafunzi wanaosoma katika shule za mijini

umeongezeka katika stadi zote kwa viwango tofauti. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa, utendaji wa wanafunzi wanaosoma katika shule zilizopo vijijini umeshuka zaidi katika stadi zote.

Katika Stadi ya Kusoma, utendaji wa wanafunzi wanaosoma katika shule zilizopo mijini umeongezeka kwa asilimia 0.78 kutoka asilimia 90.81 ya wanafunzi wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 91.59 katika upimaji wa mwaka 2018. Katika stadi hiyo, utendaji wa wanafunzi wanaosoma katika shule za vijijini umepungua kwa asilimia 2.97 kutoka asilimia 89.68 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 86.71 mwaka 2018.

Katika Stadi ya Kuandika utendaji wa wanafunzi wanaosoma katika shule zilizopo mijini umeongezeka kwa asilimia 2.04 kutoka asilimia 88.38 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 90.42 mwaka 2018. Kwa upande wa wanafunzi wanaosoma katika shule zilizopo vijijini, utendaji wao umeshuka kwa asilimia 3.54 kutoka asilimia 89.57 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 86.03 mwaka 2018.

Kushuka kwa utendaji wa wanafunzi kumejitokeza zaidi katika Stadi ya Kuhesabu kwa asilimia 10.39 kwa wanafunzi wanaosoma katika shule za vijijini na umeongezeka kwa asilimia 5.45 kwa wanafunzi wanaosoma shule zilizopo mijini. Takwimu zinaonesha kuwa, utendaji wa wanafunzi wanaosoma katika shule zilizopo mijini umeongezeka kutoka asilimia 75.33 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 80.78 mwaka 2018. Kwa upande wa wanafunzi wanaosoma katika shule za vijijini, utendaji wao ulishuka kutoka asilimia 79.49 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 69.10 mwaka 2018. Chati Na. 4 inaonesha ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi wanaosoma katika shule za vijijini na wale wanaosoma katika shule za mijini.



**Chati Na. 4:** Utendaji wa wanafunzi wa shule za Vijijini na Shule za Mijini

Chati Na. 4 inaonesha kuwa utendaji wa wanafunzi wanaosoma katika shule za mijini ni mzuri zaidi kuliko wa wanafunzi wanaosoma katika shule zilizopo vijijini.

### **6.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kutoka katika Shule Zilizofanya upimaji Mara ya Kwanza 2018 na zilizorudia Upimaji mara ya Pili 2018**

Katika kufanya sampuli ya mikoa, halmashauri na shule zilizohusika katika upimaji, shule 33 zilizokuwa zimefanya upimaji mwaka 2017 zilijumuishwa katika sampuli ili ziweze kurudia upimaji kwa mara nyingine. Aidha, shule 33 nyingine mpya ziliongezwa ili kukamilisha shule 66 zilizokuwa zinahitajika kwenye sampuli.


Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kutoka katika shule zilizokuwa zinarudia upimaji mwaka 2018 na zile zilizokuwa zinafanya kwa mara ya kwanza ulifanyika. Lengo la kufanya ulinganifu huu lilikuwa kuona kama walimu kutoka katika shule zilizofanya upimaji mwaka 2017 walifaidika kwa kupata maarifa ya namna upimaji unavyofanyika pamoja na mapendekezo

yaliyotolewa katika taarifa za mwaka 2017 hivyo kuwawezesha kubadilisha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji.

Takwimu zinaonesha kuwa, wanafunzi wanaosoma katika shule ambazo zimefanya upimaji kwa mara ya kwanza mwaka 2018 walikuwa na utendaji mzuri zaidi ikilinganishwa na wanafunzi wanaosoma katika shule zilizofanya upimaji kwa mara ya pili. Matokeo haya yameshabihiana na ya upimaji wa mwaka 2017 ambapo, utendaji wa wanafunzi kutoka katika shule zilizofanya upimaji kwa mara ya kwanza mwaka 2017 ulikuwa mzuri zaidi ikilinganishwa na wanafunzi waliofanya upimaji mwaka 2015 ambapo mwaka 2017 walifanya upimaji kwa mara ya pili.

Katika Stadi ya Kusoma, utendaji wa wanafunzi wanaosoma katika shule zilizofanya upimaji kwa mara ya kwanza, asilimia 90.62 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana ikilinganishwa na asilimia 88.71 ya wanafunzi wanaosoma katika shule zilizofanya upimaji kwa mara ya pili wenye utendaji kama huo. Aidha, katika Stadi ya Kuandika, wanafunzi wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana walikuwa asilimia 91.19 ikilinganishwa na asilimia 88.05 ya wanafunzi wenye utendaji kama huo kutoka katika shule zilizofanya upimaji kwa mara ya pili.

Mwelekeo unaofanana na huo ulionekana pia kwenye Stadi ya Kuhesabu ambapo asilimia 79.83 ya wanafunzi waliotoka katika shule zilizofanya upimaji kwa mara ya kwanza walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana ikilinganishwa na asilimia 74.69 ya wanafunzi kutoka katika shule zilizofanya upimaji kwa mara ya pili. Chati Na. 5 inaonesha muhtasari wa takwimu hizo.



**Chati Na. 5:** Utendaji wa Wanafunzi katika Shule Zilizofanya Upimaji mwaka 2017 na 2018


Chati Na. 5 inaonesha kuwa, kuna tofauti ndogo kati ya shule zilizofanya upimaji kwa mara ya kwanza mwaka 2018 na shule zilizofanya kwa mara ya pili ambapo wanafunzi waliotoka katika shule zilizofanya upimaji kwa mara ya kwanza wameonesha kuwa na utendaji mzuri zaidi ikilinganishwa na wanafunzi wanaotoka katika shule zinazofanya upimaji kwa mara ya pili.

### 6.6 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule 33 zilizofanya Upimaji mwaka 2017 na Kurudia mwaka 2018

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi katika shule 33 zilizofanya upimaji mwaka 2017 na kurudia upimaji mwaka 2018 umefanyika.

Matokeo ya uchambuzi wa takwimu yanaonesha kuwa, utendaji wa wanafunzi waliofanya upimaji mwaka 2018 umeongezeka katika stadi zote tatu ikilinganishwa na utendaji wa wanafunzi wa shule hizo waliofanya upimaji mwaka 2017. Takwimu zinaonesha kuwa, katika Stadi ya Kusoma, asilimia 92.03 ya wanafunzi waliofanya upimaji mwaka 2018 walikuwa na utendaji mzuri zaidi ikilinganishwa na asilimia 88.71 ya wanafunzi waliofanya upimaji mwaka 2017 katika shule hizo. Vilevile, asilimia 90.53 ya wanafunzi waliofanya upimaji mwaka 2018 katika Stadi ya Kuandika walikuwa na utendaji mzuri zaidi ikilinganishwa na

asilimia 88.05 ya wanafunzi waliofanya upimaji mwaka 2017 katika shule hizo. Hali kadhalika, asilimia 80.82 ya wanafunzi waliofanya upimaji mwaka 2018 katika Stadi ya Kuhesabu walikuwa na utendaji mzuri zaidi ikilinganishwa na asilimia 74.69 ya wanafunzi katika shule hizo waliofanya upimaji mwaka 2017. Muhtasari wa takwimu za ulinganifu huu zimeoneshwa katika Chati Na. 6.



**Chati Na. 6:** Ulinganifu wa Matokeo ya Wanafunzi katika Shule 33 zilizofanya Upimaji mwaka 2017 na Kurudia 2018

Chati Na. 6 inaonesha ongezeko chanya la utendaji wa wanafunzi waliofanya upimaji mwaka 2018 ikilinganishwa na utendaji wa wanafunzi waliofanya upimaji mwaka 2017. Ongezeko la wanafunzi wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa mwaka 2018 katika shule zilizofanya upimaji kwa miaka yote miwili (2017 na 2018) linaonesha kuwa, ushiriki wa shule hizo ulisaidia kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

## 7.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Stadi ya Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ulifanyika kwa lengo la kubaini utendaji wa wanafunzi

katika kila stadi na dhana zilizopimwa. Aidha, uchambuzi wa majibu ulifanyika ili kubaini changamoto zilizowakabili wanafunzi kwa lengo la kutoa ushauri kwa mamlaka husika ili ziweze kufanyiwa kazi ipasavyo na hivyo kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK.

### **7.1 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Stadi ya Kusoma**

Umahiri wa wanafunzi katika Stadi ya Kusoma umechambuliwa kwa kuzingatia vigezo vya utendaji wa wanafunzi katika usomaji wa maneno, sentensi na kifungu cha maneno. Uchambuzi wa umahiri wa wanafunzi katika Stadi ya Kusoma swali la kwanza na la pili ulitegemea idadi ya maneno mwanafunzi aliyoweza kusoma na swali la tatu kigezo kilikuwa idadi ya maswali aliyoweza kujibu kwa usahihi.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulifanyika kwa kuzingatia vigezo vya utendaji katika usomaji wa maneno, sentensi na kifungu cha maneno. Katika kusoma maneno, mwanafunzi alihesabika kuwa na **utendaji hafifu**, kama alishindwa kusoma maneno yote au aliweza kusoma neno 1 hadi maneno 6 tu kati ya maneno 25. Mwanafunzi aliyeweza kusoma maneno 7 hadi 13 alihesabika kuwa na **utendaji wa wastani**. Kwa upande mwingine, mwanafunzi aliyeweza kusoma maneno 14 hadi 19 alikuwa na **utendaji mzuri** na mwanafunzi aliyeweza kusoma maneno 20 hadi 25 ndani ya dakika moja alikuwa na **utendaji mzuri sana**. Kigezo hicho kilitumika pia katika kubainisha utendaji wa wanafunzi katika umahiri wa kusoma sentensi, ambapo utendaji wa mwanafunzi ulipimwa kutokana na idadi ya maneno aliyoweza kusoma katika sentensi hizo zilizokuwa na jumla ya maneno 25.

Katika swali la 3 utendaji wa mwanafunzi ulitegemea uwezo wa kusoma kifungu cha maneno kisha kujibu maswali manne yaliyotokana na kifungu cha maneno alichokisoma kwa sauti kwa muda wa dakika tatu. Mwanafunzi aliyeshindwa kujibu maswali yote au aliyeweza kujibu swali moja tu kwa usahihi alihesabika kuwa na **utendaji hafifu**. Mwanafunzi aliyeweza kujibu maswali mawili alikuwa na **utendaji wa wastani** wakati mwanafunzi aliyeweza kujibu maswali matatu alikuwa na

**utendaji mzuri.** Aidha, mwanafunzi aliyejibu maswali yote manne kwa usahihi alikuwa na **utendaji mzuri sana.**

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Stadi ya Kusoma unaonesha kuwa, wanafunzi wengi walikuwa na utendaji mzuri sana katika swali la 2 ikilinganishwa na maswali mengine. Takwimu za matokeo zinaonesha kuwa, wanafunzi 4,627 sawa na asilimia 82.32 walikuwa na utendaji mzuri sana kwani waliweza kusoma maneno kati ya 20 hadi 25. Mfano wa majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno yote katika sentensi zote umeoneshwa katika Kielelezo Na. 1.

<p>2. Kusoma sentensi (alama 25)</p> <p>Weka alama ya mkwaju (/) kwa kila neno katika sentensi ambalo mwanafunzi ameshindwa kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia (Ø) neno hilo. (Kila neno moja sahihi alama 1)</p> <p>_____</p> <p>Mbuzi wangu wana mikia mifupi.</p> <p>_____</p> <p>Njoo hapa dada yangu mpole.</p> <p>_____</p> <p>Tafadhali fungua kitabu chako vizuri.</p> <p>_____</p> <p>Viatu vyangu vyote ni vyeusi.</p> <p>_____</p> <p>Hawa ni watoto wadogo sana.</p>	<p>2. Reading of the sentences (25 marks)</p> <p>Put a stroke mark (/) in all words in a sentence which the pupil has failed to read. Circle (Ø) if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed (The score for each correct word is 1 mark)</p> <p>My goats have short tails.</p> <p>Come here my calm sister.</p> <p>Please, open your book carefully.</p> <p>All my shoes are black.</p> <p>These are very young children.</p>
---	--

**Kielelezo Na. 1** kinaonesha Skeli ya Upimaji ambapo wanafunzi waliweza kusoma sentensi zote tano zenye maneno 25 ndani ya muda uliopangwa.

Uchambuzi zaidi wa takwimu katika swali hili unaonesha kuwa, wanafunzi waliokuwa na utendaji mzuri (maneno 14 hadi 19) walikuwa 291 sawa na asilimia 5.18 wakati wanafunzi 170 sawa na asilimia 3.02 walikuwa na utendaji wa wastani (maneno 7 hadi 13). Aidha, wanafunzi 533 sawa na asilimia 9.48 walikuwa na utendaji hafifu (maneno 0 hadi 6). Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa, wanafunzi 335 sawa na asilimia 5.96 walishindwa kusoma maneno yote katika sentensi zote. Kielelezo Na. 2 kinaonesha majibu ya baadhi ya wanafunzi walioshindwa kusoma maneno yote katika sentensi.



<p>2. Kusoma sentensi (alama 25)</p> <p>Weka alama ya mkwaju (/) kwa kila neno katika sentensi ambalo mwanafunzi ameshindwa kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia (Ø) neno hilo. (Kila neno moja sahihi alama 1)</p> <p><u>Mbyazi wangu wana mikia mifupi.</u></p> <p><u>Njoo hapa dada yangu mbole.</u></p> <p><u>Tafadhali jungua kitabu chako vizuri.</u></p> <p><u>Vitatu vyangu vyote ni vyazusi.</u></p> <p><u>Hawa ni watoto wadogo sana.</u></p>	<p>2. Reading of the sentences (25 marks)</p> <p>Put a stroke mark (/) in all words in a sentence which the pupil has failed to read. Circle (Ø) if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed (The score for each correct word is 1 mark)</p> <p><u>My goats have short tails.</u></p> <p><u>Come here my calm sister.</u></p> <p><u>Please, open your book carefully.</u></p> <p><u>All my shoes are black.</u></p> <p><u>These are very young children.</u></p>
--	---

**Kielelezo Na. 2** kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kusoma sentensi zote tano.

Swali lililofuatia kuwa na wanafunzi wengi wenye kiwango kizuri sana cha utendaji ni swali la 1. Utendaji wa wanafunzi katika kusoma maneno ulikuwa wa wastani hadi mzuri sana kwani asilimia 89.91 ya wanafunzi waliweza kusoma maneno 7 hadi 25 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na. 5: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno**

Maneno	Utendaji	Idadi	Asilimia
0 – 6	Hafifu	567	10.09
7 – 13	Wastani	238	4.23
14 – 19	Mzuri	414	7.37
20 – 25	Mzuri Sana	4,402	78.31
	<b>Jumla</b>	<b>5,621</b>	<b>100.00</b>

Jedwali Na. 5 linaonesha kuwa, jumla ya wanafunzi 4,402 sawa na asilimia 78.31 walikuwa na utendaji mzuri sana kwa kuweza kusoma maneno 20 hadi 25 kwa ufasaha. Idadi hiyo ya maneno ni zaidi ya robo tatu ya maneno yote waliyotakiwa kusoma katika swali hili. Kielelezo Na. 3 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno yote kwa usahihi.

<p>1. Kusoma maneno (alama 12<sup>1</sup>/<sub>2</sub>)</p> <p>Weka alama ya mkwaju (/) kwa kila neno ambalo mwanafunzi ameshindwa kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kwa usahihi, zungushia (Ø) neno hilo. (Kila neno moja sahihi alama 00<sup>1</sup>/<sub>2</sub>)</p> <p>televisheni    gita    vitamini    Wiki    Picha  kompyuta    pini    mdomo    sentensi    nyumba  tochi    baiskeli    mwanafunzi    ubao    mwavuli  chumvi    saa    mbwa    mwezi    kikombe  mchele    mkono    mwanga    karoti    jogoo</p>	<p>1. Reading of words (12<sup>1</sup>/<sub>2</sub> marks)</p> <p>Put a slanted slash mark (/) in each word which the pupil has failed to read. Circle (Ø) if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed. (The score for each correct word is 00<sup>1</sup>/<sub>2</sub> mark)</p> <p>television    guitar    vitamins    week    picture  computer    pin    mouth    sentence    house  torch    bicycle    pupil    blackboard    umbrella  salt    watch    dog    moon    cup  rice    arm    light    carrot    cock</p>
--	--

**Kielelezo Na. 3** kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma kwa ufasaha maneno yote 25 kwa muda wa dakika moja.

Takwimu pia zinaonesha kuwa, wanafunzi 414 sawa na asilimia 7.37 walikuwa na utendaji mzuri ambapo waliweza kusoma maneno kati ya 14 hadi 19 na wanafunzi 238 (4.23%) walikuwa na utendaji wa wastani kwa kuweza kusoma maneno kati ya 7 hadi 13. Aidha, wanafunzi 567 sawa na asilimia 10.09 walikuwa na utendaji hafifu. Kati yao, asilimia 4.86 waliweza kusoma kati ya neno 1 hadi maneno 6 na asilimia 5.23 hawakuweza kusoma neno lolote. Kielelezo Na. 4 kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kusoma maneno yote.

<p>1. Kusoma maneno (alama 12<sup>1/2</sup>)</p> <p>Weka alama ya mkwaju (/) kwa kila neno ambalo mwanafunzi ameshindwa kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kwa usahihi, zungushia (Ø) neno hilo. (Kila neno moja sahihi alama 00<sup>1/2</sup>)</p> <p>televisi sheni   gita   vitamini   Wjki   Picha  kompyuta   pini   mdomo   senjensi   nyumba  tochi   baiskeli   mwanafunzi   ubao   mwawuli  chumvi   saa   mbywa   mwezi   kikombe  mchele   mkono   mwanga   karoti   jogobo</p>	<p>1. Reading of words (12<sup>1/2</sup> marks)</p> <p>Put a slanted slash mark (/) in each word which the pupil has failed to read. Circle (Ø) if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed. (The score for each correct word is 00<sup>1/2</sup> mark)</p> <p>television   guitar   vitamins   wpek   picture  computer   pin   month   sentence   house  torch   bicycle   pupil   blackboard   umbrella  salt   watch   dog   moon   cup  rice   arm   light   carrot   cock</p>
---	--

**Kielelezo Na. 4** ni sampuli ya majibu ya wanafunzi ambao hawakuweza kusoma neno lolote kati ya maneno 25.

Katika swali la 3 lililohusu kusoma kifungu cha maneno, asilimia 71.20 ya wanafunzi walikuwa na utendaji mzuri hadi mzuri sana baada ya kujibu kwa usahihi maswali yasiyopungua matatu. Kati yao, asilimia 46.79 walikuwa na utendaji mzuri sana na asilimia 24.41 walikuwa na utendaji mzuri. Wanafunzi hao walikuwa na uwezo wa kusoma kifungu cha maneno na kukielewa vizuri na kisha kujibu maswali kwa usahihi. Muhtasari wa matokeo ya utendaji katika swali hili umeoneshwa katika Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na. 6: Utendaji wa Wanafunzi katika Kujibu Maswali baada ya Kusoma Kifungu cha Maneno**

Idadi ya Vipengele	Viwango vya Utendaji	Idadi ya Wanafunzi	Asilimia ya Wanafunzi
1	Hafifu	986	17.54
2	Wastani	633	11.26
3	Mzuri	1,372	24.41
4	Mzuri sana	2,630	46.79
	<b>Jumla</b>	<b>5,621</b>	<b>100.00</b>

Uchambuzi wa takwimu za majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi 4,635 (82.46%) walionesha utendaji wa wastani hadi

mzuri sana. Kwa upande mwingine wanafunzi 986 walikuwa na utendaji hafifu ambapo kati yao, 681 (12.12%) hawakuweza kujibu kipengele chochote cha swali lolote kwa usahihi. Kielelezo Na. 5 ni mfano wa majibu ya wanafunzi walioweza kujibu swali la 3 kwa usahihi.

Maswali na Majibu			Questions and Answers		
Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi kuanzia kipengele (a) hadi (c) zungushia alama 3 na kipengele (d) alama 3½, iwapo atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama 0 na kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali lifuatalo.			If a pupil will give a correct answer, circle 3 marks for letter (a) up to (c) and 3½ marks for letter (d), if he/she will give an incorrect answer, circle the 0 mark and then write the total marks in the space provided in the table.		
No	Maswali na majibu	alama	No.	Question and Answer	Marks
(a)	Furaha ana umri wa miaka mingapi? (nane)	3 0	(a)	How old is Furaha? (Eight years)	3 0
(b)	Furaha anaishi na nani? (kaka yake mkubwa)	3 0	(b)	Who lives with Furaha? (Her elder brother)	3 0
(c)	Furaha alikwenda wapi siku ya Jumatatu? (dukani)	3 0	(c)	Where did Furaha go on Monday? (To the shop)	3 0
(d)	Furaha alitumiaje shilingi mia tano aliyokuwa nayo? (alinunulia penseli mbili na kifutio)	3½ 0	(d)	How did Furaha spend her five hundred shilings? (She used it to buy two pencils and an eraser)	3½ 0

**Kielelezo Na. 5** kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kujibu vipengele vyote vya swali kwa usahihi baada ya kusoma kifungu cha maneno.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walishindwa kujibu maswali yaliyotokana na kifungu cha maneno walichosoma, hivyo kuwa na utendaji hafifu. Mfano wa majibu ya wanafunzi walioshindwa kutoa majibu sahihi umeoneshwa katika Kielelezo Na. 6.


Maswali na Majibu			
Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi kuanzia kipengele (a) hadi (c) zungushia alama 3 na kipengele (d) alama 3½, iwapo atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama 0 na kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali			
No	Maswali na majibu	alama	
(a)	Furaha ana umri wa miaka mingapi? (nane)	3	0
(b)	Furaha anaishi na nani? (kaka yake mkubwa)	3	0
(c)	Furaha alikwenda wapi siku ya Jumatatu? (dukani)	3	0
(d)	Furaha alitumiaje shilingi mia tano aliyokuwa nayo? (alinunulia penseli mbili na kifutio)	3½	0

Questions and Answers			
If a pupil will give a correct answer, circle 3 marks for letter (a) up to (c) and 3½ marks for letter (d), if he/she will give an incorrect answer, circle the 0 mark and then write the total marks in the space provided in the table.			
No.	Question and Answer	Marks	
(a)	How old is Furaha? (Eight years)	3	0
(b)	Who lives with Furaha? (Her elder brother)	3	0
(c)	Where did Furaha go on Monday? (To the shop)	3	0
(d)	How did Furaha spend her five hundred shilings? (She used it to buy two pencils and an eraser)	3½	0

**Kielelezo Na. 6** kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu maswali yote ya ufahamu baada ya kusoma kifungu cha maneno.

Ulinganifu wa takwimu za utendaji katika Stadi ya Kusoma umeonesha kuwa, wanafunzi waliojibu swali la 3 walikuwa na utendaji wa chini zaidi ikilinganishwa na maswali mengine. Chati Na. 7 inaonesha umahiri wa wanafunzi katika swali la 1, la 2 na la 3.



**Chati Na. 7:** Utendaji wa Wanafunzi katika kila Swali Katika Stadi ya Kusoma

Chati Na. 7 inaonesha wanafunzi wana utendaji mzuri zaidi katika swali la 2 (kusoma sentensi) likifuatiwa na swali la 1 (kusoma maneno). Aidha, utendaji wa wanafunzi ulikuwa wa kiwango cha chini katika swali la tatu ikilinganishwa na maswali mengine.

## 7.2 Uchambuzi wa Takwimu katika Majibu ya Wanafunzi katika Stadi ya Kuandika

Idadi ya wanafunzi waliofanya upimaji katika Stadi ya Kuandika ilikuwa 5,677 sawa na asilimia 81.77 ya wanafunzi 6,941 waliosajiliwa kufanya upimaji wa KKK 2018. Upimaji katika stadi hii ulihusu umahiri wa wanafunzi katika kutambua picha za vitu na kuandika majina ya vitu hivyo, kutambua maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa na ndogo na uwezo wa kunakili

kifungu cha maneno na kutumia alama za uandishi katika kifungu cha maneno.





















Vigezo vya utendaji kwa swali la 1 vilizingatia uwezo wa mwanafunzi kutambua na kuandika majina ya vitu vilivyooneshwa kwenye picha (umahiri wa uundaji wa maneno). Mwanafunzi aliyeweza kuandika majina 9 hadi 10 alihesabika kuwa na **utendaji mzuri sana**; aliyeweza kuandika majina 6 hadi 8 **utendaji mzuri**; aliyeweza kuandika majina 3 hadi 5 **utendaji wa wastani** na aliyeweza kuandika majina ya picha zisizozidi mbili alihesabika kuwa na **utendaji hafifu**.

Katika swali la 2 (uumbaji wa herufi) mwanafunzi alikuwa amepewa jumla ya maneno 20. Kati ya hayo, maneno 10 yaliandikwa kwa herufi kubwa. Mwanafunzi alitakiwa kubainisha maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa kwa kuyapigia mstari. Mwanafunzi aliyeweza kupigia mstari maneno 9 hadi 10 yaliyoandikwa kwa herufi kubwa alikuwa na **utendaji mzuri sana**; Mwanafunzi aliyeweza kupigia mstari maneno 6 hadi 8 alikuwa na **utendaji mzuri**. Mwanafunzi aliyeweza kupigia mstari maneno 3 hadi 5 alikuwa na **utendaji wa wastani** na mwanafunzi aliyepigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa chini ya matatu alikuwa na **utendaji hafifu**.

Katika swali la 3 lililokuwa na alama 20, mwanafunzi aliyeweza kunakili maneno 13 hadi 16 na kutumia alama 4 za uandishi kwa usahihi alihesabika kuwa na **utendaji mzuri sana**. Aidha aliyeweza kunakili maneno 11 hadi 15 na kuweka alama 3 za uandishi kwa usahihi alihesabika kuwa na **utendaji mzuri** na **utendaji wa wastani** aliyenakili maneno 6 hadi 10 na kuweka alama 2 za uandishi. Endapo mwanafunzi aliweza kunakili maneno yasiyozidi manne na kuweka alama moja tu ya uandishi, alitathminiwa kuwa na **utendaji hafifu**.

Takwimu za matokeo zinaonesha kuwa, wanafunzi waliofanya vizuri katika swali la 1 kwa kuwa na kiwango cha utendaji mzuri hadi mzuri sana ni asilimia 72.85. Kati yao, asilimia 27.00 walionesha utendaji mzuri sana.

Wanafunzi walioonesha utendaji mzuri waliweza kuandika majina 6 hadi 8 yanayowakilisha vitu vilivyooneshwa katika picha zote kwa usahihi. Aidha wanafunzi walioonesha kiwango cha juu zaidi cha utendaji waliandika kwa usahihi majina ya picha 9 hadi 10 jambo linaloonesha kuwa walikuwa na uwezo mzuri wa kuandika maneno. Mfano wa majibu ya wanafunzi hao yameoneshwa katika Kielelezo Na. 7.





















1. Tazama kwa makini picha zifuatazo kisha andika majina yake katika nafasi zilizo wazi.		. Study the pictures below carefully and then write their names in the spaces provided.	
(a)  ki-su	(b)  Piki Piki	(a)  Knife	(b)  Motorcycle
(c)  Helikopta	(d)  CHUPE	(c)  Helicopter	(d)  Bottle
(e)  JANZOO	(f)  kuku	(e)  Millipede	(f)  Hen
(g)  Kikabu	(h)  ki nyasa	(g)  Book	(h)  Chameleon
(i)  panja	(j)  Samaki	(i)  Rat	(j)  Fish

**Kielelezo Na. 7** kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kuandika majina yanayowakilisha kila picha kwa usahihi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliokuwa na kiwango hafifu cha utendaji katika swali hilo ni asilimia 10.78. Baadhi ya wanafunzi hao waliweza kuandika majina ya picha za vitu viwili pekee wakati wengine hawakuweza kuandika jina la picha yoyote. Aidha, wapo wanafunzi wengine walionakili maneno kutoka katika swali la 2 lililohusu kupigia mstari maneno yenye herufi kubwa na kuyafanya kuwa majibu katika baadhi ya picha.



Mfano wa majibu ya wanafunzi walioshindwa kuandika majina yanayowakilisha vitu vilivyo katika picha yameoneshwa katika Kielelezo Na. 8.

1. Tazama kwa makini picha zifuatazo kisha andika majina yake katika nafasi zilizo wazi.		1. Study the pictures below carefully and then write their names in the spaces provided.	
(a)  MKATE	(b)  chuNgwa	(a)  panga	(b)  Motta
(c)  hulima	(d)  KiJi ko	(c)  Anapite	(d)  bott
(e)  BLUV	(f)  KiJo hi	(e)  An daga	(f)  Heni
(g)  NYE KUNDU	(h)  Ma nJa ho	(g)  _____	(h)  _____
(i)  SAA	(j)  mku Ki	(i)  u - o -	(j)  o - o -

**Kielelezo Na. 8** kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kuandika majina ya vitu vyote vilivyooneshwa katika picha. Mwanafunzi aliyejibu kwa lugha ya Kiswahili alitumia baadhi ya maneno kutoka swali la 2.

Katika swali la 2, asilimia 70.74 ya wanafunzi waliweza kutambua na kisha kupigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa kuanzia 6 hadi 10, yaani utendaji mzuri hadi mzuri sana. Kati yao asilimia 60.28 walifanya vizuri zaidi kwa kupigia mstari maneno 9 hadi 10 jambo linaloonesha kuwa walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu matumizi ya herufi kubwa na ndogo

katika uandishi. Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kujibu swali hilo kwa usahihi imeoneshwa katika Kielelezo Na. 9.

<p>2. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa.</p> <p>(a) <u>MKATE</u>, chungwa, mlima, <u>KIJIKO</u></p> <p>(b) <u>BLUU</u>, kijani, <u>NYEKUNDU</u>, manjano</p> <p>(c) <u>SAA</u>, mkuki, <u>CHAKI</u>, karatasi</p> <p>(d) Paka, <u>SIMBA</u>, pundamilia, <u>NYANI</u></p> <p>(e) <u>SHATI</u>, sketi, <u>GAUNI</u>, suruali</p>	<p>2. Underline the words which are written in capital letters.</p> <p>(i) <u>BREAD</u>, orange, mountain, <u>SPOON</u></p> <p>(ii) <u>BLUE</u>, green, <u>RED</u>, yellow</p> <p>(iii) <u>WATCH</u>, spear, <u>CHALK</u>, paper</p> <p>(iv) Cat, <u>LION</u>, zebra, <u>MONKEY</u></p> <p>(v) <u>SHIRT</u>, skirt, <u>DRESS</u>, trousers</p>
--	--

**Kielelezo Na. 9** kinaonesha wanafunzi walioweza kubaini na kupigia mstari maneno yote yaliyoandikwa kwa herufi kubwa.

Uchambuzi wa takwimu umeonesha kuwa, asilimia ndogo (5.94%) ya wanafunzi walionesha utendaji wa kiwango cha wastani na kuwepo kwa wanafunzi waliokuwa na kiwango hafifu cha utendaji katika swali hilo kwa asilimia 23.32. Wanafunzi walioonesha kiwango hicho cha chini walishindwa kutambua angalau maneno mawili yaliyoandikwa kwa herufi kubwa na kuyapigia mstari, hivyo baadhi yao walipigia mstari maneno ya herufi ndogo. Wengine walipigia mstari maneno yote, jambo linaloonesha kuwa, hawakuwa na uwezo wa kutofautisha dhana ya herufi kubwa na ndogo. Mfano wa majibu ya wanafunzi hao umeoneshwa katika Kielelezo Na. 10.

<p>2. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa.</p> <p>(a) <u>MKATE</u>, chungwa, mlima, <u>KIJIKO</u></p> <p>(b) <u>BLUU</u>, kijani, <u>NYEKUNDU</u>, manjano</p> <p>(c) <u>SAA</u>, mkuki, <u>CHAKI</u>, karatasi</p> <p>(d) Paka, <u>SIMBA</u>, pundamilia, <u>NYANI</u></p> <p>(e) <u>SHATI</u>, sketi, <u>GAUNI</u>, suruali</p>	<p>2. Underline the words which are written in capital letters.</p> <p>(i) <u>BREAD</u>, orange, mountain, <u>SPOON</u></p> <p>(ii) <u>BLUE</u>, green, <u>RED</u>, yellow</p> <p>(iii) <u>WATCH</u>, spear, <u>CHALK</u>, paper</p> <p>(iv) <u>Cat</u>, <u>LION</u>, zebra, <u>MONKEY</u></p> <p>(v) <u>SHIRT</u>, skirt, <u>DRESS</u>, trousers</p>
--	---

**Kielelezo Na. 10** kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyepigia mstari maneno yote, badala ya kupigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa na aliyepigia mstari herufi ndogo badala ya herufi kubwa.

Katika swali la 3 lililohusu kifungu cha maneno, mwanafunzi alitakiwa kunakili kifungu hicho na kisha kuweka alama za uandishi. Alama hizo ni nukta (.), mkato (,), mshangao (!) na alama ya kuuliza (?). Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 20. Asilimia 69.49 ya wanafunzi waliojibu swali hilo walikuwa na utendaji mzuri hadi mzuri sana. Kati yao, asilimia 42.33 walionesha utendaji mzuri sana kutokana na kuweza kunakili maneno 13 hadi 16 kwa usahihi na kutumia alama 4 za uandishi kwa usahihi. Wanafunzi waliokuwa na kiwango kizuri cha utendaji walinakili maneno 11 hadi 15 na kuweka alama 3 za uandishi kwa usahihi. Kielelezo Na. 11 kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kunakili kifungu chote na kuweka alama husika za uandishi kwa usahihi.

<p>3. Nakili kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: nukta (.), mkato (,), alama ya kushangaa (!), na alama ya kuuliza (?) mahali panapostahili.</p> <p>Jamani eeh_ Basi la kwenda nyumbani kwetu limetuacha_ Sasa je_ tutaondoka na usafiri wa basi gani_?</p> <p><u>Jamani eeh! Basi la kwenda nyumbani kwetu limetuacha. Sasa je, tutaondoka na usafiri wa basi gani?</u></p>	<p>3. Copy the following paragraph in the space given and then put the punctuation marks: full stop (.), comma (,), exclamation mark (!) and question mark (?) where necessary.</p> <p>My goodness _ The bus has already left _ So _ which bus are we going to travel by _</p> <p><u>My goodness! The bus has already left.</u></p> <p><u>So, which bus are we going to</u></p> <p><u>travel by?</u></p>
---	--

**Kielelezo Na. 11** kinaonesha wanafunzi walioweza kunakili na kuonesha alama zote za uandishi sehemu husika.


Takwimu za matokeo ya viwango vya utendaji wa wanafunzi katika swali hili zinaonesha kuwa, asilimia 21.30 walikuwa na utendaji hafifu kutokana na kushindwa kunakili kifungu cha maneno na kuweka angalau alama moja ya uandishi. Baadhi ya wanafunzi hao hawakuweza kunakili kifungu cha maneno wala kuweka alama sahihi mahali husika; na wengine kutoweka alama yoyote ya uandishi mahali zilipotakiwa. Aidha, kati ya wanafunzi walioshindwa kunakili kifungu cha maneno, baadhi yao

walikosea tahajia na wengine waliandika bila kuacha nafasi kati ya neno moja na jingine. Pia baadhi ya wanafunzi waliandika maneno mengine tofauti na yaliyopo katika kifungu cha maneno walichopewa. Wapo pia wanafunzi walioweza kunakili kifungu cha maneno kama ilivyotakiwa kwenye maelekezo ya swali lakini walishindwa kuweka alama za uandishi sehemu stahiki. Kielelezo Na. 12 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kuweka alama za uandishi sehemu stahiki.

<p>3. Nakili kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: nukta (.), mkato (,), alama ya kushangaa (!), na alama ya kuuliza (?) mahali panapostahili.</p>	<p>Copy the following paragraph in the space given and then put the punctuation marks: full stop (.), comma (,), exclamation mark (!) and question mark (?) where necessary.</p>
<p>Jamani eeh__ Basi la kwenda nyumbani kwetu limetuacha__ Sasa je__ tutaondoka na usafiri wa basi gani__</p>	<p>My goodness __ The bus has already left __ So __ which bus are we going to travel by __</p>
<p><u>Ja maniech, Basi lakwenda nyumbani kwetu limetuacha. Sasa je? tutaondoka na usafiri wa basi gani.</u></p>	<p><u>My goodness, The bus has already left? So which bus are we going to travel by!</u></p>

**Kielelezo Na. 12** ni majibu ya wanafunzi walioshindwa kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama stahiki kwa usahihi. Wanafunzi hao waliandika silabi/maneno yasiyolingana na kifungu cha maneno.

Takwimu za ulinganifu wa utendaji kati ya wanafunzi kwa kila swali katika Stadi ya Kuandika umeoneshwa katika Chati Na. 8.



**Chati Na. 8** inaonesha Viwango vya Utendaji wa wanafunzi katika Kila Swali katika Stadi ya Kuandika

Chati Na. 8 inaonesha kuwa, asilimia ya wanafunzi waliokuwa na umahiri mzuri sana ilikuwa ndogo zaidi katika swali la 3 kuliko swali la 1 na la 2. Katika swali la 1 na la 2 wanafunzi waliokuwa na utendaji mzuri sana walikuwa asilimia 27.00 na asilimia 60.28 wakati katika swali la tatu wanafunzi waliokuwa na umahiri mzuri sana walikuwa asilimia 42.33.

Kwa ujumla, matokeo ya upimaji wa mwaka 2018 yanaonesha kuwa katika Stadi ya Kuandika, wanafunzi walifanya vizuri zaidi katika **umahiri wa Uumbaji** wa Herufi katika swali la 2 (kubaini maneno yenye herufi kubwa) ambapo asilimia 60.28 walikuwa na utendaji mzuri sana. Katika umahiri wa **Uundaji wa Maneno** (swali la 1 kuandika majina ya picha), wanafunzi wachache walikuwa na utendaji mzuri sana (27.00%). Aidha, asilimia 45.85 walikuwa na utendaji mzuri. Umahiri wa matumizi ya kanuni za Uandishi (swali la 3) ulikuwa asilimia 42.33 ambao uko juu kuliko wa swali la 1 ikilinganishwa na mwaka 2017. Utendaji wa wanafunzi katika umahiri wa Uundaji wa Maneno umepungua kutoka asilimia 51.57 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 27.00 kwa mwaka 2018. Aidha, umahiri wa Uumbaji wa

Herufi nao umeshuka kidogo kutoka asilimia 60.38 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 60.28 katika upimaji wa mwaka 2018. Hata hivyo takwimu zinaonesha kuwa, umahiri katika Kanuni za Uandishi umeongezeka kutoka asilimia 30.32 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi asilimia 42.33 katika upimaji wa mwaka 2018 ambapo kumekuwa na ongezeko la asilimia 12.

### **7.3 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Stadi ya Kuhesabu**

Wanafunzi 5,682 sawa na asilimia 81.9 walifanya upimaji katika Stadi ya Kuhesabu. Karatasi ya upimaji ilikuwa na jumla ya maswali 20 ambayo yalipima umahiri wa Kutambua Dhana ya Namba, Matendo katika Namba na Kutambua uhusiano wa Vitu na Namba. Dhana ya Matendo katika Namba ilihusisha kujumlisha kwa hatua ya 1 na 2; na kutoa hatua ya 1 na 2 kwa tarakimu zisizozidi 3. Hivyo kiwango cha umahiri katika kila stadi kilitegemea idadi ya maswali aliyoweza kuyajibu mwanafunzi. Upimaji wa utendaji wa wanafunzi kwa kila umahiri ulitumia vigezo vinne ambavyo ni **utendaji hafifu** kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali yasiyozidi mawili (2); **utendaji wa wastani** kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali matatu (3); **utendaji mzuri** kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali manne (4) na **utendaji mzuri** sana kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali yote matano (5).

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, wanafunzi walifanya vizuri zaidi katika umahiri wa Kujumlisha ikifuatiwa na Kutambua Dhana ya Namba, hasa namba zinazokosekana katika mfululizo. Utendaji wa wanafunzi katika Umahiri wa Matendo ya Namba hususan tendo la kutoa ulikuwa hafifu ikilinganishwa na tendo la kujumlisha pamoja na kubaini namba zinazokosekana katika mfululizo wa namba. Aidha wanafunzi walikuwa na utendaji wa chini zaidi katika hesabu za mafumbo.

**Jedwali Na. 7: Utendaji wa Wanafunzi katika Dhana Mbalimbali**

Dhana iliyopimwa	Utendaji wa Wanafunzi							
	Hafifu		Wastani		Mzuri		Mzuri sana	
	Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
Mfululizo wa Namba	2,098	36.92	1,176	20.70	953	16.77	1,455	25.61
Kujumlisha	1,800	31.68	1,117	19.66	1,427	25.11	1,338	23.55
Kutoa	2,646	46.57	1,404	24.71	1,025	18.04	607	10.68
Kufumbua Mafumbo	3,157	55.56	1,031	18.15	906	15.95	588	10.35

**Jedwali Na. 7** linaonesha umahiri wa wanafunzi katika dhana mbalimbali katika Stadi ya Kuhesabu.

Takwimu katika Jedwali Na. 7 zinaonesha kuwa, katika dhana zilizopimwa, wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika tendo la kujumlisha kwa asilimia 68.32. Wanafunzi hao waliweza kujumlisha kwa usahihi kuanzia swali la 3 hadi la 5 yaliyotumika katika kupima umahiri huo. Wanafunzi walioweza kubaini namba 3 hadi 5 zinazokosekana katika mfululizo (utendaji wa wastani hadi mzuri sana) walikuwa asilimia 63.08 ikilinganishwa na asilimia 68.32 ya wanafunzi katika kundi hilo katika dhana ya kujumlisha.

Utendaji mzuri sana wa asilimia 25.61 ulioneshwa na wanafunzi katika kutambua namba zinazokosekana katika mfululizo wa namba ambao umepungua kwa asilimia 0.16 ikilinganishwa na upimaji wa mwaka 2017. Kwa upande mwingine, umahiri wa kubaini namba 3 hadi 5 zinazokosekana katika mfululizo wa namba (utendaji wa wastani hadi mzuri sana) umeongezeka kwa asilimia 4.98 ikilinganishwa na upimaji wa 2017.

Sampuli ya majibu ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi maswali yote 5 yaliyopima umahiri wa namba zinazokosekana katika mfululizo wa namba imeoneshwa katika Kielelezo Na. 13.



Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi.	Write the missing number:
1. 4, 5, <u>6</u> , 7, 8, 9.	1. 4, 5, <u>6</u> , 7, 8, 9. 
2. 15, <u>14</u> , 13, 12, 11.	2. 15, <u>14</u> , 13, 12, 11. 
3. 44, 46, <u>48</u> , 50, 52.	3. 44, 46, <u>48</u> , 50, 52. 
4. 70, 80, 90, <u>100</u> .	4. 70, 80, 90, <u>100</u> . 
5. 25, 30, <u>35</u> , 40, 45.	5. 25, 30, <u>35</u> , 40, 45. 

**Kielelezo Na. 13** ni majibu ya wanafunzi walioweza kubaini namba zinazokosekana na kuziandika katika nafasi husika.

Takwimu zinaonesha pia kuwa, wapo wanafunzi ambao walishindwa kujibu kwa usahihi maswali yote matano. Kati yao wapo wanafunzi walioandika namba kwa kubahatisha jambo linaloonesha kuwa hawakuwa na uelewa wa kanuni ya kutumia kupata namba sahihi. Wengine walitumia tendo la kujumlisha au kutoa baadhi ya namba katika mfululizo uliotolewa na kuandika jibu lisilo sahihi kwenye nafasi iliyo wazi. Kielelezo Na. 14 kinaonesha mfano wa majibu hayo.

Write the missing number:	Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi.
1. 4, 5, <u>15</u> , 7, 8, 9. $8+7=15$	1. 4, 5, <u>13</u> , 7, 8, 9.
2. 15, <u>1</u> , 13, 12, 11. $13-12=1$	2. 15, <u>14</u> , 13, 12, 11.
3. 44, 46, <u>90</u> , 50, 52. $46+44=90$	3. 44, 46, <u>50</u> , 50, 52.
4. 70, 80, 90, <u>17</u> . $90+80=17$	4. 70, 80, 90, <u>260</u> .
5. 25, 30, <u>15</u> , 40, 45. $30-25=15$	5. 25, 30, <u>35</u> , 40, 45.


**Kielelezo Na. 14:** Majibu ya wanafunzi walioshindwa kubaini namba sahihi zinazokosekana katika swali la 1 hadi la 5. Mwanafunzi aliyejibu kwenye karatasi ya lugha ya Kiingereza alitumia matendo ya namba kupata jibu husika kimakosa.



Uchambuzi zaidi umeonesha kuwa, katika mfululizo wa namba, wanafunzi wengi, (4,709) sawa na asilimia 82.88 waliweza kujibu kwa usahihi swali la 1 lililokuwa na mfululizo wa namba unaoongezeka kwa namba moja. Swali hilo lilifuatiwa na swali la 4 ambalo lilihusu mfululizo wa namba unaoongezeka kwa kumi ambapo wanafunzi 4,034 sawa na asilimia 71.00 waliweza kujibu.

Katika swali la 2 lililohusu mfululizo wa namba unaopungua kwa namba moja, wanafunzi waliweza kujibu kwa usahihi walikuwa 3,780 sawa na asilimia 66.53. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa, wanafunzi wengi walishindwa swali la 3 na la 5 ambayo yalikuwa na mfululizo unaoongezeka kwa namba mbili na tano mtawalia. Kwa mujibu wa takwimu za utendaji, wanafunzi 2,316 sawa na asilimia 40.76 waliweza kujibu swali la 5 kwa usahihi na wanafunzi 1,994 sawa na asilimia 35.09 waliweza kujibu kwa usahihi swali la 3.


Takwimu hizi zinaonesha kuwa wanafunzi walipata changamoto ya kutambua namba inayokosekana katika mfululizo wa namba zinazopungua na namba zinazoongezeka kwa 2 na kwa 5 isipokuwa zilizokuwa zinaongezeka kwa 10. Muhtasari wa takwimu za utendaji katika swali la 1 hadi la 5 umeoneshwa katika Chati Na. 9.



**Chati Na. 9:** Utendaji wa Wanafunzi katika Umahiri Mahsusi wa Utambuzi wa Namba.

Utendaji wa wanafunzi katika kujumlisha namba zenye tarakimu zisizozidi tatu ulipimwa katika swali la 6 hadi la 10. Maswali hayo yalikusisha kujumlisha namba mbili zenye tarakimu moja moja, kujumlisha namba mbili; moja yenye tarakimu mbili na nyingine yenye tarakimu moja bila kubeba; kujumlisha namba mbili, moja yenye tarakimu moja na nyingine yenye tarakimu mbili kwa kubeba mara moja na kujumlisha namba mbili zenye tarakimu mbili kila moja kwa kubeba mara moja pamoja na kujumlisha fedha.

Muhtasari wa takwimu za matokeo ya utendaji wa wanafunzi kwa kila swali lililopima umahiri wa kujumlisha namba upo katika Chati Na. 10.



**Chati Na.10:** Utendaji wa Wanafunzi katika Umahiri mahsusi wa Kujumlisha.

Takwimu katika Chati Na. 10 zinaonesha kuwa, asilimia 89.63 ya wanafunzi walikuwa na utendaji mzuri zaidi katika kujumlisha namba mbili zenye tarakimu moja katika swali la 6 likifuatiwa na swali la 7. Katika swali la 7 asilimia 75.47 ya wanafunzi walikuwa na utendaji mzuri katika kujumlisha namba yenye tarakimu mbili na namba yenye tarakimu moja. Kielelezo Na. 15 ni mfano wa majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu swali la 6 mpaka la 10 kwa usahihi.

Tafuta Majibu:	Work out the answers:
6. $1 + 7 =$ <u>8</u>	6. $1 + 7 =$ <u>8</u>
7. $12 + 5 =$ <u>17</u>	7. $12 + 5 =$ <u>17</u>
8. $28 + 6 =$ <u>34</u>	8. $28 + 6 =$ <u>34</u>
9. $47 + 16 =$ <u>63</u>	9. $47 + 16 =$ <u>63</u>
10. Shilingi 400 + shilingi 50 = <u>shilingi 450</u>	10. 400 shillings + 50 shillings = <u>450 shillings</u>

**Kielelezo Na. 15** ni sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kujibu swali la 6 hadi la 10 kwa usahihi.

Hata hivyo, umahiri wa wanafunzi ulipungua katika kujumlisha namba zilizohitaji kubeba kutoka mamoya kwenda makumi. Kwa mfano, katika swali la 8 lililouliza  $28 + 6 =$ , baadhi ya wanafunzi waliandika majibu kama vile 24 na wengine 214 badala ya 34. Pia, katika swali la 9 lililouliza  $47 + 16 =$ , baadhi ya wanafunzi waliandika majibu kama vile 513,53 na wengine 43 badala ya 63.

Changamoto hiyo imetokana na ama wanafunzi kushindwa kubeba makumi au kutozingatia utaratibu wa uandishi wa namba katika nafasi ya mamoya na makumi. Aidha, wanafunzi 3,257 sawa na asilimia 57.32 walipata changamoto zaidi katika swali la 10 lililohusu kujumlisha fedha ikilinganishwa na maswali mengine kwani katika swali hili walitakiwa kupanga vizuri namba walizopewa kwa usahihi katika mamoya, makumi na mamia kabla ya kujumlisha fedha hizo. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi walipata jibu 900 na wengine 40,050 badala ya 450 kutokana na kushindwa kupanga namba kwa usahihi kabla ya kuzijumlisha. Changamoto hii imepungua ikilinganishwa na upimaji wa mwaka 2017 iliyokuwa na asilimia 61.99. Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali la 8 hadi la 10 imeoneshwa kwenye Kielelezo Na. 16.

Tafuta Majibu:

6.  $1 + 7 = \underline{8}$

7.  $12 + 5 = \underline{17}$

8.  $28 + 6 = \underline{24}$

9.  $47 + 16 = \underline{513}$

10. Shilingi 400 + shilingi 50 = 900

**Kielelezo Na. 16** ni jibu la mwanafunzi aliyepanga namba 50 katika mamia badala ya kupanga katika makumi, hivyo kupata jibu 900 badala ya 450.

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa, wanafunzi 431 sawa na asilimia 7.58 walikuwa na utendaji hafifu kutokana na kushindwa kujibu kwa usahihi maswali yote matano. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alijibu kwa kuunganisha takwimu za namba alizopaswa kujumlisha katika swali la 7 na alikuwa akijaribu kufanya hivyo katika swali la 8. Aidha mwanafunzi mwingine alitumia tendo la kutoa katika swali la 8. Kielelezo Na. 19 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi waliotoa majibu yasiyo sahihi katika swali la 6 hadi 10.

Tafuta Majibu:

6.  $1 + 7 = \underline{38}$

7.  $12 + 5 = \underline{215}$

8.  $28 + 6 = \underline{826}$

9.  $47 + 16 = \underline{11471}$

10. Shilingi 400 + shilingi 50 = 40020

Work out the answers:

6.  $1 + 7 = \underline{3}$

7.  $12 + 5 = \underline{4}$

8.  $28 + 6 = \underline{22}$

9.  $47 + 16 = \underline{33}$

10. 400 shillings + 50 shillings = 400

**Kielelezo Na.17** kinaonesha majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali la 6 hadi la 10.

Umahiri wa wanafunzi katika kutoa namba zenye tarakimu zisizozidi tatu ulipimwa katika swali la 11 hadi 15. Uchambuzi wa takwimu za matokeo katika umahiri wa kutoa unaonesha kuwa, wanafunzi 2,647 sawa na asilimia 46.57 walikuwa na

utendaji hafifu. Jumla ya wanafunzi 3,037 sawa na asilimia 53.43 waliweza kujibu maswali matatu hadi matano kwa usahihi. Wanafunzi 1,405 sawa na asilimia 24.72 walikuwa na utendaji wa wastani na 1,025 sawa na asilimia 18.03 walikuwa na utendaji mzuri. Wanafunzi waliokuwa na utendaji mzuri sana walikuwa ni wachache zaidi (10.68%) ikilinganishwa na utendaji mwingine. Kielelezo Na. 18 kinaonesha majibu ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi swali la 11 hadi la 15.

11. $8 - 5 =$ <u>3</u>	11. $8 - 5 =$ <u>3</u>
12. $19 - 4 =$ <u>15</u>	12. $19 - 4 =$ <u>15</u>
13. $25 - 7 =$ <u>18</u>	13. $25 - 7 =$ <u>18</u>
14. $67 - 18 =$ <u>49</u>	14. $67 - 18 =$ <u>49</u>
15. Shilingi 700 - shilingi 550 = <u>shilingi 150</u>	15. 700 shillings - 550 shillings = <u>150 shillings</u>

**Kielelezo Na. 18** ni majibu ya wanafunzi walioweza kujibu swali la 11 hadi la 15 kwa usahihi.

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa, swali la 11 liliongoza kwa kufanyika vizuri likifuatiwa na swali la 12 kwa asilimia 75.82 na 64.20 mtawalia. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi waliojibu vizuri swali la 11 waliweza kutoa namba mbili, moja yenye tarakimu mbili na nyingine tarakimu moja. Matokeo hayo hayatofautiani sana na ya upimaji wa mwaka 2017 ambapo swali la 11 liliongoza kwa kufanyika vizuri likifuatiwa na swali la 12 kwa asilimia 72.14 na 66.46 mtawalia. Hii inaonesha kuwa, dhana ya kutoa kwa kuchukua pamoja na hesabu za fedha bado inawashinda wanafunzi wengi.

Utendaji wa wanafunzi katika umahiri wa kutoa namba zinazohitaji dhana ya kuchukua uliopimwa katika swali la 13, 14 na 15 ulikuwa ni asilimia 54.38, 31.19 na 21.52 mtawalia. Hii inaonesha kuwa, utendaji wa wanafunzi ulipungua katika maswali ya kutoa na kwa kadiri idadi ya tarakimu

ilivyoongezeka. Kielelezo Na. 19 kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu swali la 13 hadi la 15.

11. $8 - 5 = \underline{3}$	11. $8 - 5 = \underline{3}$
12. $19 - 4 = \underline{15}$	12. $19 - 4 = \underline{15}$
13. $25 - 7 = \underline{18}$	13. $25 - 7 = \underline{28}$
14. $67 - 18 = \underline{59}$	14. $67 - 18 = \underline{44}$
15. $700 \text{ shillings} - 550 \text{ shillings} = \underline{\text{Shillings } 150}$	15. $\text{Shilingi } 700 - \text{shilingi } 550 = \underline{250}$

**Kielelezo Na. 19** ni majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu swali la 13 hadi la 5. Wanafunzi wote walikosa umahiri wa kuchukua katika swali la 15.

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa, utendaji wa wanafunzi katika Umahiri wa kufumbua mafumbo ulikuwa wa wastani isipokuwa swali la 20 lililokuwa na utendaji hafifu (20.59%). Maswali yaliyokuwa na utendaji wa wastani, utendaji ulikuwa katika mtiririko wa swali la 16 lenye asilimia 51.18, swali la 19 asilimia 49.54, swali la 17 asilimia 47.41 na swali la 18 asilimia 45.88. Matokeo ya utendaji katika matendo ya namba yaliyotumika katika umahiri huo yameoneshwa katika Jedwali Na. 8.

#### **Jedwali Na. 8. Utendaji wa Wanafunzi katika Kufumbua Mafumbo**

<b>Namba ya Swali</b>	<b>Tendo la Namba</b>	<b>Idadi ya Wanafunzi waliopimwa</b>	<b>Idadi ya waliojibu kwa usahihi</b>	<b>Asilimia</b>
16	Kujumlisha	5,682	2,908	51.18
17	Kutoa	5,682	2,695	47.43
18	Kujumlisha	5,682	2,607	45.88
19	Kujumlisha	5,682	2,815	49.54
20	Kutoa	5,682	1,170	20.59

**Jedwali Na. 8** linaonesha utendaji katika matendo ya namba yaliyotumika katika umahiri wa kufumbua mafumbo.

Hata hivyo umahiri wa kufumbua mafumbo hasa yanayohusisha tendo la kutoa umeongezeka kutoka asilimia 18.19 katika upimaji wa mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 20.59 katika upimaji wa mwaka 2018 jambo linaloonesha kuwa, kuna juhudi ambazo zimefanyika katika kutatua changamoto inayojitokeza katika umahiri huu.

Kwa upande mwingine, zaidi ya nusu ya wanafunzi (55.54%) walikuwa na utendaji hafifu. Miongoni mwao asilimia 26.59 walishindwa kujibu kwa usahihi maswali yote. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa sababu zilizochangia wanafunzi kuwa na utendaji hafifu ni pamoja na:

- (a) Wanafunzi kushindwa kutumia kwa usahihi matendo ya kujumlisha au kutoa. Kwa mfano, katika swali la 16, 18 na 19 baadhi ya wanafunzi walitoa badala ya kujumlisha namba walizopewa. Hali kadhalika, katika swali la 17 na 20 wanafunzi wengine walijumlisha badala ya kutoa namba zilizotolewa. Jambo hilo linaonesha kwamba walishindwa kuelewa maana ya maneno kama vile “alibakiwa na”, “jumla” yaliyotumika katika maswali.
- (b) Wanafunzi kunakili maswali yaliyotolewa badala ya kukokotoa majibu; kutokujibu maswali na wengine kuandika majibu yasiyoeleweka.
- (c) Wanafunzi kufanya makosa wakati wa kujumlisha au kutoa hali iliyosababisha kupata majibu yasiyo sahihi.

Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali la 16 hadi la 20 imeoneshwa kwenye Kielelezo Na. 20.

16. Mary ana machungwa 240 na kaka yake ana machungwa 342. Je, jumla wana machungwa mangapi?

$$\begin{array}{r} \text{Mary ana machungwa } 240 \text{ na kaka yake ana machungwa } \\ 342 \text{ Je jumla wana machungwa mangapi?} \\ \hline \text{machungwa } 240 \\ \text{machungwa } - 342 = 102 \end{array}$$

17. Sara alikuwa na pipi 450. Alimgawia rafiki yake pipi 220. Je, alibakiwa na pipi ngapi?

$$\begin{array}{r} \text{Sara alikuwa na pipi } 450 \text{ Alimgawia rafiki yake pipi } 220 \\ \text{Je, alibakiwa na pipi ngapi?} \\ \hline 450 \\ + 220 \\ \hline 630 \end{array}$$

18. Darasa la pili lina wasichana 70 na wavulana 90. Je, darasa hilo lina wanafunzi wangapi?

$$\begin{array}{r} \text{Darasa la pili lina wasichana } 70 \text{ na wavulana } 90 \text{ Je,} \\ \text{darasa hilo lina wanafunzi wangapi?} \\ \hline 70 \\ + 90 \\ \hline 170 \end{array}$$

19. Juma alinunua kalamu kwa shilingi 150 na daftari kwa shilingi 500. Je, alilipa shilingi ngapi?

$$\begin{array}{r} \text{Juma alinunua kalamu kwa shilingi } 150 \text{ na daftari} \\ \text{kwa shilingi } 500 \text{ Je, alilipa shilingi ngapi?} \\ \hline 150 \\ - 500 \\ \hline 650 \end{array}$$

20. Musa alipewa shilingi 600 na baba yake. Alitumia shilingi 250. Je, alibakiwa na shilingi ngapi?

$$\begin{array}{r} \text{Musa alipewa shilingi } 600 \text{ na baba yake Alitumia} \\ \text{shilingi } 250 \text{ Je, alibakiwa na shilingi ngapi?} \\ \hline 600 \\ - 250 \\ \hline 450 \end{array}$$

**Kielelezo Na. 20:** Majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali la 16 hadi la 20.



Hata hivyo, pamoja na utendaji wa wastani katika umahiri huo, wapo wanafunzi waliokuwa na utendaji mzuri baada ya kuweza kujibu maswali yote kwa usahihi. Sampuli ya majibu hayo imeoneshwa kwenye Kielelezo Na. 21.

16. Mary ana machungwa 240 na kaka yake ana machungwa 342. Je, jumla wana machungwa mangapi?

$$\begin{array}{r} 240 \\ + 342 \\ \hline 582 \end{array}$$

jumla ana machungwa 582

17. Sara alikuwa na pipi 450. Alimgawia rafiki yake pipi 220. Je, alibakiwa na pipi ngapi?

$$\begin{array}{r} 450 \\ - 220 \\ \hline 230 \end{array}$$

alibakiwa na pipi 230

18. Darasa la pili lina wasichana 70 na wavulana 90. Je, darasa hilo lina wanafunzi wangapi?

$$\begin{array}{r} 70 \\ + 90 \\ \hline 160 \end{array}$$

jumla darasa lina wanafunzi 160

19. Juma alinunua kalamu kwa shilingi 150 na daftari kwa shilingi 500. Je, alilipa shilingi ngapi?

$$\begin{array}{r} 150 \\ + 500 \\ \hline 650 \end{array}$$

jumla ni shilingi 650

20. Musa alipewa shilingi 600 na baba yake. Alitumia shilingi 250. Je, alibakiwa na shilingi ngapi?

$$\begin{array}{r} 600 \\ - 250 \\ \hline 350 \end{array}$$

alibakiwa na shilingi 350

**Kielelezo Na. 21:** Majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali la 16 hadi 20. Mwanafunzi aliweza kutumia matendo ya kujumlisha na kutoa katika maswali husika.

## **8.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA USIMAMIZI**

Baraza la Mitihani liliandaa dodoso zilizotumika wakati wa upimaji kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK. Dodoso hilo pia lililenga kupata maoni yenye kuboresha changamoto zinazoendelea kujitokeza. Aidha lililenga kubaini hali ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK ili kuweza kutoa ushauri kwa lengo la kuboresha kiwango cha Elimu inayotolewa katika ngazi hiyo.

Katika kupata taarifa husika, aina mbili za dodoso zilitumika: moja iliyokamilishwa na walimu wakuu 66 na nyingine wasimamizi 696 waliosimamia upimaji wa stadi za KKK. Taarifa zilizohitajika katika dodoso hizo ni pamoja na ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi, mahudhurio ya wanafunzi katika kila stadi, ujuzi wa walimu katika kufundisha stadi za KKK na uwepo wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Taarifa nyingine ni hali ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wa Darasa la I na la II kwa mwaka 2019.

### **8.1 Taarifa za Shule kwa Ujumla**

Dodoso la Mwalimu Mkuu lililenga kupata taarifa kuhusu uwepo wa mihtasari ya ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK. Lengo lilikuwa kubaini ikiwa ufundishaji na ujifunzaji unazingatia taratibu kama zilivyoainishwa katika mtaala wa elimumsingi.

Uchambuzi wa majibu ya dodoso umebainisha kuwa, shule zote 66 zilizohusika katika upimaji wa mwaka 2018 sawa na asilimia 100, zilikuwa na mihtasari ya kufundishia Stadi za KKK kwa Darasa la Kwanza na la Pili ikilinganishwa na asilimia 98.2 ya mwaka 2017. Takwimu hizi zinaonesha kuwa juhudi za makusudi zilifanyika kuwezesha shule zote zilizohusika katika upimaji wa mwaka 2018 kuwa na mihtasari ya kufundishia Stadi za KKK.

Uchambuzi zaidi ulifanyika ili kupata taarifa kuhusu idadi ya mikondo na idadi ya wanafunzi katika kila mkondo. Umuhimu wa taarifa hii ulikuwa kuona kama idadi ya ukomo ya wanafunzi 40 kwa mkondo kama iliyoelekezwa katika Mtaala wa Elimu ya

Msingi Tanzania 2007 inazingatiwa. Majibu ya Walimu Wakuu yameoneshwa katika Jedwali Na.9.

**Jedwali Na. 9: Idadi ya Wanafunzi katika Mkondo**

Na.	Mfiko wa Idadi ya Wanafunzi	Idadi ya Shule Darasa la I		Idadi ya Shule Darasa la II	
		Idadi	%	Idadi	%
1.	9 - 40	42	63.6	41	62.1
	41 - 50	5	7.6	3	4.5
2.	51 - 60	4	6	4	6
3.	61 - 70	1	1.5	2	3
4.	71 - 80	3	4.5	6	9.1
5.	81 - 90	2	3	1	1.5
6.	91- 100	4	6	1	1.5
7.	101+	5	7.6	8	12.1

**N= 66**

Jedwali Na. 9 linaonesha kuwa, shule 42 sawa na asilimia 63.6 zilikuwa na mikondo yenye idadi ya wanafunzi kwa ukomo ulioelekezwa katika darasa la I na shule 41 sawa na asilimia 62.1 zilikuwa na idadi hiyo kwa darasa la II. Takwimu hizo zinaonesha kuwa, idadi kubwa ya shule za msingi zilizohusika katika upimaji wa stadi za KKK 2018 hazikuwa na msongamano mkubwa wa wanafunzi katika vyumba vya madarasa. Kwa takwimu hizo, shule 25 sawa na asilimia 37.9 zilikuwa na mikondo yenye wanafunzi zaidi ya idadi inayokubalika kwa darasa la II na shule 24 sawa na asilimia 36.2 kwa darasa la I. Kati ya shule zilizokuwa na msongamano wa wanafunzi darasani, nane, sawa na asilimia 12.1 kwa darasa la II na 5 (7.6%) darasa la I zilikuwa na mikondo yenye wanafunzi zaidi ya 100.

Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa, kwa shule zinazotumia mfumo wa lugha ya kiingereza shule moja ilikuwa na mikondo yenye wanafunzi zaidi ya 40 kwa darasa la I. Uchambuzi zaidi wa madodoso unaonesha kuwa, sababu za baadhi ya shule kuwa na mikondo yenye idadi kubwa ya wanafunzi ni uchache wa vyumba vya madarasa na uhaba wa walimu wanaofundisha stadi za KKK.

Takwimu hizi zinaonesha kuwa, bado kuna changamoto ya msongamano wa wanafunzi wa darasa la I na la II hivyo juhudi za makusudi zinahitajika kuondoa changamoto hiyo.

## **8.2 Ufundishaji wa Wanafunzi na Mafunzo kwa Walimu wa Stadi za KKK**

Dodoso la Mwalimu Mkuu kupata taarifa za ufundishaji na mafunzo kwa walimu wa stadi za KKK. Takwimu zinaonesha kuwa, Shule zote 66 sawa na asilimia 100 zilizofanya upimaji zilikuwa na angalau mwalimu mmoja anayefundisha katika darasa la I na II. Hata hivyo, taarifa hizo zinaonesha kuwa kati ya walimu 178 wanaofundisha Stadi za KKK katika shule hizo, walimu 71 sawa na asilimia 39.89 walikuwa wamepata mafunzo maalum kwa ajili ya ufundishaji wa stadi husika.

Takwimu zinaonesha kuwa, asilimia ya walimu wenye mafunzo ya KKK walioshiriki katika upimaji wa mwaka 2018 imepungua sana ikilinganishwa na asilimia 81.9 katika upimaji wa mwaka 2017. Upungufu huo umetokana na upimaji wa mwaka 2018 kuhusisha walimu wa madarasa ya juu (III-VII) wakati upimaji wa mwaka 2017 ulihusisha walimu wa madarasa ya I na II tu.

## **8.3 Hali ya Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

Walimu wakuu waliulizwa kuhusu upatikanaji wa vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia kama vile vitabu vya kiada, ziada na vifaa vingine vinavyotumika kufundishia kila Stadi. Majibu ya walimu hao yameainishwa katika Jedwali Na.16.

**Jedwali Na. 10: Upatikanaji wa Vitabu na Vifaa vya Kujifunzia KKK**

Na.	Hoja	Idadi	Idadi ya waliojibu	%
(a)	Upatikanaji wa Vitabu vya kiada vya kufundishia Stadi za Kuhesabu	66	62	93.9
(b)	Upatikanaji wa vitabu vya ziada vya mazoezi ya Stadi ya Kuhesabu	66	57	86.4
(c)	Uwepo wa Vifaa vya kufundishia Stadi ya Kuhesabu, kama vile vihesabio	66	61	92.4
(d)	Uwepo wa vitabu vya kiada na Vifaa vya kufundishia Stadi ya Kuandika	66	56	87.9
(e)	Uwepo wa vitabu vya kiada vya kufundishia Stadi ya Kusoma	66	61	92.4
(f)	Upatikanaji wa vifaa vinavyolenga kuendeleza Stadi ya Kusoma	66	59	89.4
(g)	Uwepo wa vitabu vya kiada vya kufundishia Stadi ya Kuandika	66	61	92.4

Jedwali Na. 10 linaonesha kuwa, upatikanaji wa vitabu vya kufundishia stadi zote katika shule zilizoteuliwa kufanya upimaji ulikuwa mzuri. Upatikanaji wa vitabu vya kiada vya Stadi ya Kuhesabu ulikuwa mzuri zaidi kwa kuwa na asilimia 93.9, Stadi ya Kuandika asilimia 92.4 na vitabu kwa ajili ya Stadi ya Kusoma asilimia 92.4. Pia uwepo wa vitabu vya ziada kwa ajili ya kufundishia Stadi ya Kuhesabu ulikuwa mzuri kwa asilimia 86.4 na vifaa vingine kwa ajili ya kukuzia umahiri wa somo hilo ulikuwa mzuri kwa asilimia 92.4. Kwa upande mwingine, upatikanaji wa vifaa kama vile vitabu vya hadithi za watoto wadogo kwa ajili ya kukuzia Stadi ya Kusoma ulikuwa mzuri (89.4%).

Takwimu hizi zinaonesha kuwa, upatikanaji wa vitabu vya kiada ulikuwa mzuri zaidi kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na mwaka 2017. Kwa mfano, mwaka 2017 upatikanaji wa vitabu vya kiada vya kufundishia Stadi ya Kuhesabu ulikuwa asilimia 93.3 wakati mwaka 2018 ulikuwa asilimia 93.9. Aidha upatikanaji wa vitabu vya ziada vya mazoezi kwa Stadi hiyo uliongezeka kutoka asilimia

85.0 mwaka 2017 hadi asilimia 86.4 mwaka 2018. Kwa upande mwingine, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia stadi hiyo uliongezeka kutoka asilimia 91.8 mwaka 2017 hadi asilimia 92.4 mwaka 2018.

Uwepo wa vitabu pamoja na zana za kufundishia na kujifunzia unaonesha juhudi kubwa za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za KKK zimefanywa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (WyEST) na Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), uongozi wa Elimu ngazi za Mikoa, Wilaya hadi Shule.

#### 8.4 Miundombinu na Mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Ili kupata taarifa kuhusu hali halisi ya mazingira ya ufundishaji, walimu wakuu walitakiwa kutoa taarifa kuhusu uwepo wa madawati, meza na viti vya kukalia wanafunzi na walimu wanaofundisha stadi za KKK. Pia waliulizwa kuhusu uwepo wa vyumba vya madarasa na upatikanaji wa chumba maalum kinachotumika kama maktaba kwa ajili ya wanafunzi na walimu kujisomea wawapo shuleni. Muhtasari wa majibu ya walimu ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 11.

**Jedwali Na. 11: Muhtasari wa Majibu ya Walimu Kuhusu Mazingira ya kujifunzia KKK**

Na.	Hoja	Idadi	Idadi ya waliojibu	%
1.	Uwepo wa madawati, meza na viti vya kukalia wanafunzi na walimu wa Darasa la I na la II shuleni.	66	56	84.8
2.	Hali ya uwepo wa vyumba vya madarasa ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wa Darasa la I na la II waliopo shuleni.	66	52	78.8
3.	Upatikanaji wa chumba maalum au maktaba ambapo watoto na walimu wanaweza kuazima vitabu ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza zaidi stadi za KKK hata baada ya muda wa shule.	66	36	54.5

Jedwali Na. 11 linaonesha kuwa, asilimia 78.8 ya walimu waliripoti kuwepo kwa vyumba vya kutosha vya madarasa na

uwepo wa samani kama vile madawati, viti na meza kwa kiwango cha asilimia 84.8. Takwimu hizo pia zinaonesha uwepo wa ongezeko dogo la samani ikilinganishwa na la mwaka 2017 ambapo zilikuwa zinapatikana kwa asilimia 84.6. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa, shule ambazo zilikuwa na maktaba au chumba maalum kwa ajili ya watoto na walimu kuweza kuazima vitabu na kuwawezesha wanafunzi kujisomea zaidi baada ya muda wa shule ni asilimia 54.5.

## 8.5 Mahudhurio ya Wanafunzi

Taarifa ya mahudhurio ya wanafunzi katika dodoso la wasimamizi zinaonesha kuwa, wanafunzi waliofanya upimaji ni 5,771 (82.04%) na idadi ya wanafunzi ambao hawakufanya upimaji kwa sababu mbalimbali ni 1,263 (17.96%). Baadhi ya sababu zilizobainishwa na wasimamizi zimeoneshwa katika Jedwali Na .12.

**Jedwali Na. 12: Taarifa za Wanafunzi Wasiofanya Upimaji**

Na	Sababu	Idadi	Asilimia
1.	Utoro	867	68.6
2.	Kuhama shule	198	15.7
3.	Kukariri (Kurudia) darasa	61	4.8
4.	Ugonjwa	25	2.1
5.	Kufariki	07	0.6
6.	Hakuna sababu iliyotolewa	105	8.6
<b>Jumla</b>		<b>1263</b>	<b>100</b>
<b>N= 1,263</b>			

Jedwali Na. 12 linaonesha kuwa, utoro ulikuwa ni sababu kubwa iliyoathiri mahudhurio ya wanafunzi katika upimaji ambapo ulikuwa asilimia 68.6. Sababu nyingine ilikuwa ni wanafunzi kuhama shule iliyokuwa na asilimia 15.7, na asilimia 4.8 walikariri darasa la pili. Baadhi ya wanafunzi (2.1) hawakujitokeza kwa sababu ya ugonjwa na asilimia 0.6 walifariki dunia. Aidha baadhi ya wasimamizi walikiri kuwepo kwa wanafunzi ambao hawakufanya upimaji (8.6%) bila kubainisha sababu ya kutohudhuria kwao.

Idadi ya wanafunzi watoro katika upimaji wa mwaka 2018 imepungua kwa asilimia 17.9 ikilinganishwa na asilimia 86.5 ya wanafunzi watoro katika upimaji wa mwaka 2017. Mafanikio hayo yanaonesha kuwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) zilishirikiana vizuri na uongozi wa Elimu ngazi za Mikoa, Wilaya hadi ngazi ya Shule pamoja na wazazi katika kupunguza changamoto hizo.

## **9.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

### **9.1 Hitimisho**

Upimaji wa stadi za KKK Darasa la II wa mwaka 2018 uliendeshwa kwa kufuata taratibu zote zilizoainishwa katika mwongozo wa uendeshaji wa upimaji huo. Katika upimaji huo, jumla ya wanafunzi 5,771 walihudhuria na kufanya upimaji huo. Kati yao, wanafunzi 1,263 sawa na asilimia 17.96 hawakufanya upimaji huo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo utoro ambao ulikuwa asilimia 68.6 ya wanafunzi ambao hawakuweza kufanya upimaji. Hata hivyo, utoro umepungua kwa zaidi ya asilimia 17.9 kutoka asilimia 86.5 mwaka 2017 hadi asilimia 68.6 mwaka 2018. Hii inaonesha kuwa, jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na mamlaka za elimu kwa ngazi mbalimbali zinaleta mafanikio.

Taarifa inaonesha kuwa, katika stadi zote, umahiri wa wanafunzi umeongezeka. Hata hivyo, umahiri wa Stadi ya Kuhesabu ulikuwa asilimia 77.49 kwa wanafunzi waliokuwa na utendaji mzuri hadi mzuri sana; ikilinganishwa na Stadi ya Kusoma (90.2%) na Kuandika (89.19%). Hivyo, ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi hiyo unahitaji kuimarishwa. Aidha, ikilinganishwa na Upimaji wa mwaka 2017, bado kunajitokeza tofauti za kiutendaji katika stadi za KKK kati ya wanafunzi kutokana na jinsi, mahali shule ilipo (mjini/kijijini) na lugha ya kufundishia (Kiingereza au Kiswahili), tofauti ambazo Baraza linaamini kuwa ni za kiufundishaji (Pedagogical). Ni matumaini ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, mamlaka husika zitafanyia kazi mapendekezo



yaliyotolewa katika taarifa hii ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji na hivyo kuongezeka kwa umahiri katika Stadi za KKK.

Taarifa hii inaonesha kuwa, yapo maboresho yaliyofanyika na hivyo kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK. Maeneo yaliyoonekana kuboreshwa ni pamoja na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vile vitabu vya kiada na ziada na vifaa vyingine vya kufundishia na kujifunzia, uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kama vile uwepo wa madawati, viti na vyumba vya madarasa, jambo linaloonesha kuwa mamlaka zinazohusika na Elimu zinafanya jitihada kubwa kuimarisha stadi za KKK.

## **9.2 Mapendekezo**

Kutokana na matokeo ya uchambuzi wa upimaji wa stadi za KKK kwa wanafunzi wa Darasa la Pili 2018, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza:

- (a) Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (WyEST) kupitia taasisi na mamlaka zake na kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) zitengeneze mkakati mahsusi unaolenga kuwawezesha walimu kuboresha ufundishaji wa Stadi ya Kuhesabu ambayo imekuwa changamoto kwa wanafunzi kwa kuwa na wastani wa utendaji wa chini ikilinganishwa na stadi nyingine kila unapofanyika upimaji. Aidha, ufuatiliaji zaidi ufanyike kwa lengo la kuimarisha Stadi za Kusoma hasa kusoma maneno yenye herufi mwambatano; na matumizi ya alama za uandishi katika Stadi ya Kuandika.
- (b) Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR- TAMISEMI) kwa kushirikiana na mamlaka za Elimu ngazi ya Mikoa na Halmashauri zote ziendelee kuimarisha ufuatiliaji na mahudhurio ya wanafunzi darasani kwa lengo la kupunguza au kumaliza kabisa tatizo la utoro wa wanafunzi ambalo bado linaendelea kujitokeza.

- (c) Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (WyEST) kupitia taasisi na mamlaka zake na kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) zifanye uchunguzi unaolenga kubaini sababu zinazofanya utendaji wa baadhi ya wanafunzi kuwa hafifu kwa kuzingatia lugha inayotumika katika kufundisha pamoja na Shule zilipo (mijini na vijijini) ili wanafunzi wote wawe na umahiri unaowiana.
- (d) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) iendeleo kuziwezesha shule za Msingi kuwa na maktaba ambazo walimu watapata fursa ya kuazima vitabu na kuwapatia wanafunzi kwa lengo la kuimarisha ujifunzaji wa stadi za KKK.
- (e) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na TAMISEMI ziangalie uwezekano wa kujenga vyumba vya madarasa katika shule zote zenye uhaba wa madarasa na kuongeza idadi ya walimu wanaofundisha stadi za KKK katika shule za msingi. Aidha, ni vema shule zote zikawa na vifaa vilivyopendekezwa katika muhtasari ili wanafunzi wote nchini wapate maarifa husika.
- (f) Upimaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu uwe endelevu ili kuweza kubaini ngazi ya umahiri iliyofikiwa na wanafunzi katika ngazi ya Darasa la I na II, kubaini changamoto na kuweka mikakati ya kutatua changamoto hizo. Lengo likiwa kuhakikisha kuwa, wanafunzi wanaoingia Darasa la Tatu wanakuwa na umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
UPIMAJI WA DARASA LA PILI**

**201**

**STADI YA KUSOMA**

*Muda: Dakika 15      Ijumaa, 12 Aprili 2019 asubuhi*

*Maelekezo*

1. *Karatasi hii ina maswali matatu (3).*
2. *Mwanafunzi anatakiwa kujibu maswali yote kwa mdomo.*
3. *Kila mwanafunzi atapimwa kwa dakika 15.*
4. *Msimamizi anatakiwa kujaza taarifa za mwanafunzi katika nafasi zilizo wazi juu ya fomu maalum ya upimaji kwa kalamu ya wino wa bluu.*
5. *Mwanafunzi atakapokuwa amemaliza kusoma, msimamizi anatakiwa kujaza alama katika fomu maalum ya upimaji kwa kutumia kalamu ya wino mwekundu.*

## *Kusoma Maneno*

*Mwongoze mwanafunzi kusoma maneno kwa kuzingatia yafuatayo:*

- (i) Mwonesheshe mwanafunzi (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia neno la kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari.*
- (ii) Mwelekeze mwanafunzi kusoma maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo.*
- (iii) Hakikisha mwanafunzi anatumia sekunde tatu tu, kusoma kila neno. Baada ya sekunde tatu mwelekeze mwanafunzi kusoma neno linalofuata.*
- (iv) Usomaji wa maneno utafanyika kwa dakika tatu, ambapo dakika moja itatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na dakika mbili zitatumiwa na msimamizi kukokotoa alama na kujaza fomu maalum ya upimaji.*

*1. Mwanafunzi asome maneno yafuatayo:*

*televisheni gita vitamini wiki picha*

kompyuta pini mdomo sentensi nyumba  
tochi Baiskeli mwanafunzi ubao mwavuli  
chumvi saa mbwa mwezi kikombe  
mchele mkono mwanga karoti jogoo

### *Kusoma Sentensi*

*Mwongoze mwanafunzi kusoma sentensi kwa kuzingatia yafuatayo:*

- (i) Mwoneshe mwanafunzi (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari.*
- (ii) Mwelekeze mwanafunzi kusoma sentensi kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo.*
- (iii) Hakikisha mwanafunzi anatumia sekunde tatu tu, kusoma neno katika sentensi. Baada ya sekunde tatu mwelekeze mwanafunzi kusoma neno linalofuata.*
- (iv) Usomaji wa sentensi zote utafanyika kwa dakika nne, ambapo dakika moja itatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na dakika*

*tatu zitatumiwa na msimamizi kukokotoa alama na kujaza fomu maalum ya upimaji.*

*2. Mwanafunzi asome sentensi zifuatazo:*

- (i) Mbuzi wangu wana mikia mifupi.*
- (ii) Njoo hapa dada yangu mpole.*
- (iii) Tafadhali fungua kitabu chako vizuri.*
- (iv) Viatu vyangu vyote ni vyeusi.*
- (v) Hawa ni watoto wadogo sana.*

### *Kusoma Kifungu cha Maneno*

*Mwongoze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa kuzingatia yafuatayo:*

- (i) Mwoneshe mwanafunzi kifungu cha maneno (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari na mweleze mwanafunzi kuwa akimaliza kusoma, utachukua karatasi yake na utamuuliza maswali yanayohusiana na kifungu cha maneno alichosoma.*

(ii) Mwelekeze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo. Mwanafunzi atakapokuwa anasoma, fuatilia usomaji wake kwa kutumia kifungu cha maneno kilichopo katika fomu maalum ya Upimaji.

(iii) Mwanafunzi akimaliza kusoma, chukua karatasi yake ya upimaji kisha muulize maswali yaliyopo katika fomu maalum ya Upimaji.

(iv) Usomaji wa kifungu cha maneno utafanyika kwa dakika nane, ambapo dakika tatu zitatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na dakika tano zitatumiwa na msimamizi kukokotoa alama na kujaza fomu maalum ya Upimaji.

3. Mwanafunzi asome kifungu cha maneno kifuatacho kisha ajibu maswali atakayoulizwa na msimamizi kwa mdomo:

Furaha ana umri wa miaka nane. Anaishi Kinondoni na kaka yake mkubwa. Mara zote

*hutunza vitu vyake vizuri. Siku ya Jumatatu, Furaha alikwenda dukanikununua Penseli. Alikuwa na shilingi mia tano mfukoni. Alinunua penseli mbili kwa shilingi mia nne. Furaha alibaki na shilingi mia moja ambazo alizitumia kununua kifutio.*



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

*Fomu Maalum ya Kujaza Alama za Mwanafunzi katika*  
*Upimaji wa Kusoma*

*Jina la Mwanafunzi* \_\_\_\_\_

*Namba ya Mwanafunzi* \_\_\_\_\_

*Jina la Shule* \_\_\_\_\_

*Wilaya* \_\_\_\_\_

*Mkoa* \_\_\_\_\_

<b><i>KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU</i></b>		
<b><i>Namba ya Swali</i></b>	<b><i>Alama</i></b>	<b><i>Saini ya Mpimaji</i></b>
<b><i>1.</i></b>		
<b><i>2.</i></b>		
<b><i>3.</i></b>		
<b><i>Jumla</i></b>		

7. Kusoma maneno (alama 12<sup>1</sup>/<sub>2</sub>)

Weka alama ya mkwaju (/) kwa kila neno ambalo mwanafunzi ameshindwa kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kwa usahihi, zungushia (Ø) neno hilo. (Kila neno moja sahihi alama 00<sup>1</sup>/<sub>2</sub>)

televisheni	gita	vitamini	Wiki	Picha
kompyuta	pini	mdomo	sentensi	nyumba
tochi	baiskeli	mwanafunzi	ubao	mwavuli
chumvi	saa	mbwa	mwezi	kikombe
mchele	mkono	mwanga	karoti	jogoo

Alama:

## 2. Kusoma sentensi (alama 25)

Weka alama ya mkwaju (/) kwa kila neno katika sentensi ambalo mwanafunzi ameshindwa kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia (Ø) neno hilo. (Kila neno moja sahihi alama 1)

---

Mbuzi wangu wana mikia mifupi.

---

Njoo hapa dada yangu mpole.

---

Tafadhali fungua kitabu chako vizuri.

---


Viatu vyangu vyote ni vyeusi.

---

Hawa ni watoto wadogo sana.

---

**Alama:**



## 3. Kusoma kifungu cha maneno kisha kujibu maswali kwa mdomo (alama 12<sup>1</sup>/<sub>2</sub>).

Sikiliza kwa makini wakati mwanafunzi anasoma kifungu cha maneno. Baada ya mwanafunzi

kusoma, chukua karatasi aliyokuwa anasoma kisha muulize maswali yaliyopo chini ya kifungu cha maneno.

Furaha ana umri wa miaka nane. Anaishi Kinondoni na kaka yake mkubwa. Mara zote hutunza vitu vyake vizuri. Siku ya Jumatatu, Furaha alikwenda dukani kununua Penseli. Alikuwa na shilingi mia tano mfukoni. Alinunua penseli mbili kwa shilingi mia nne. Furaha alibaki na shilingi mia moja ambazo alizitumia kununua kifutio.

### **Maswali na Majibu**

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi kuanzia kipengele (a) hadi (c) zungushia alama 3 na kipengele (d) alama  $3\frac{1}{2}$ , iwapo atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama 0 na kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali lifuatalo:

<i>Na</i>	<i>Maswali na majibu</i>	<i>alama</i>	
<i>(a)</i>	<i>Furaha ana umri wa miaka mingapi? (nane)</i>	<i>3</i>	<i>0</i>
<i>(b)</i>	<i>Furaha anaishi na nani? (kaka yake mkubwa)</i>	<i>3</i>	<i>0</i>
<i>(c)</i>	<i>Furaha alikwenda wapi siku ya Jumatatu? (dukani)</i>	<i>3</i>	<i>0</i>
<i>(d)</i>	<i>Furaha alitumiaje shilingi mia tano aliyokuwa nayo? (alinunulia penseli mbili na kifutio)</i>	<i>3<sup>1</sup>/<sub>2</sub></i>	<i>0</i>
<i>Jumla ya Alama</i>			

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**  
**NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF**  
**TANZANIA**  
**STANDARD TWO ASSESSMENT**

**201**                      **READING SKILLS**

**Time: 15 Minutes      Friday, 12<sup>th</sup> April 2019 morning**

---

**Instructions**

1. *This paper has three (3) questions.*
2. *Pupils should answer all questions orally.*
3. *Every pupil will be assessed for 15 minutes.*
4. *The invigilator is required to fill in the pupil's information on the blank spaces at the top of the Assessment form by using a blue pen.*
5. *When the pupil has finished reading, the invigilator is required to fill in the marks on the special assessment form by using a red pen*

## *Reading of Words*

*Guide the pupil to read words by considering the following:*

- (i) Show the pupil (by pointing with a pen) starting from the first word from left to the right in each row.*
- (ii) Instruct the pupil to read words loudly, carefully and as quickly as possible.*
- (iii) Make sure that the pupil use **only three seconds** in reading each word. After three seconds, instruct the pupil to read the next word.*
- (iv) Reading of words will take **three minutes**, of which **one minute** will be used by the pupil to read and **two minutes** will be used by the invigilator to calculate marks and fill in the assessment form.*

1. The pupils should read the following words:

television    guitar    vitamins    week    picture

computer    pin    mouth    sentence    house

torch    bicycle    pupil    blackboard    umbrella

salt    watch    dog    moon    cup

rice    arm    light    carrot    cock

### *Reading of Sentences*

*Guide the pupil to read the sentences by considering the following:*

- (i) Show the pupil (by pointing with a pen) starting from the first sentence from left to right in each row.*
- (ii) Instruct the pupil to read the sentence loudly, carefully and as quickly as possible.*
- (iii) Make sure that the pupil uses **only three seconds** in reading each word in the sentence. After three seconds, instruct the pupil to read the next word.*



(iv) Reading of all sentences will be done for four minutes, in which one minute will be used by the pupil to read and three minutes will be used by the invigilator to calculate marks and fill in the assessment form.

2. The pupil should read the following sentences:

(i) My goats have short tails.

(ii) Come here my calm sister.

(iii) Please, open your book carefully.

(iv) All my shoes are black.

(v) These are very young children.

### **Reading of a paragraph**

Guide the pupil to read the paragraph by considering the following:

(i) Show the pupil the paragraph (by pointing with a pen) starting from the first sentence from left to right in each row and

*instruct the pupil that when he/she has finished reading, you will take his/her paper and ask him/her questions which are related to the paragraph.*

*(ii) Instruct the pupil to read the paragraph loudly, carefully and as quickly as possible. When the pupil is reading, trace his/her reading by using the paragraph which is in the assessment form.*

*(iii) When the pupil has finished reading, take his/her assessment paper and ask him/her questions which are in the special assessment form.*

*(iv) Reading of the paragraph will take eight minutes, in which three minutes will be used by the pupil to read and five minutes will be used by the invigilator to calculate marks and fill in the assessment scale paper.*

3. *The pupil should read the following paragraph and answer the questions which will be asked by the invigilator orally:*

*Furaha is eight years old. She lives at Kinondoni with her elder brother. She always keeps her things properly. On Monday, Furaha went to the shop to buy pencils. She had five hundred shillings in her pocket. She bought two pencils for four hundred shillings. Furaha remained with one hundred shillings which she used to buy an eraser.*

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**  
**NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA**  
*The Special Form to Fill in Pupil's Marks for Reading  
Assessment*

*Name of the Pupil* \_\_\_\_\_

*Pupil's Number* \_\_\_\_\_

*Name of the School* \_\_\_\_\_

*District* \_\_\_\_\_

*Region* \_\_\_\_\_

<b>FOR ASSESSOR'S USE ONLY</b>		
<b>Question Number</b>	<b>Marks</b>	<b>Assessor's Signature</b>
4.		
5.		
6.		
<b>Total</b>		

1. Reading of words (12½ marks)

Put a slanted slash mark (/) in each word which the pupil has failed to read. Circle (Ø) if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed. (The score for each correct word is 00½ mark)

television    guitar    vitamins    week    picture

computer    pin    mouth    sentence    house

torch    bicycle    pupil    blackboard    umbrella

salt    watch    dog    moon    cup

rice    arm    light    carrot    cock

Marks:

2. Reading of the sentences (25 marks)

Put a stroke mark (/) in all words in a sentence which the pupil has failed to read. Circle (Ø) if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed (The score for each correct word is 1 mark)

*My goats have short tails.*

*Come here my calm sister.*

*Please, open your book carefully.*

*All my shoes are black.*

*These are very young children.*

**Marks:**

Reading of the paragraph and answering the questions orally (12½ marks)

Listen carefully while the pupil is reading the paragraph. When he/she has finished reading, collect the paper which the pupil was reading and then ask him/her the questions from the paragraph.

Furaha is eight years old. She lives at Kinondoni with her elder Brother. She always keeps her things properly. On Monday, Furaha went to the shop to buy pencils. She had five hundred shillings in her pocket. She bought two pencils for four hundred shillings. Furaha remained with one hundred shillings which she used to buy an eraser.

## Questions and Answers

If a pupil will give a correct answer, circle 3 marks for letter (a) up to (c) and  $3\frac{1}{2}$  marks for letter (d), if he/she will give an incorrect answer, circle the 0 mark and then write the total marks in the space provided in the table.

No.	Question and Answer	Marks	
(a)	How old is Furaha? (Eight years)	3	0
(b)	Who lives with Furaha? (Her elder brother)	3	0
(c)	Where did Furaha go on Monday? (To the shop)	3	0
(d)	How did Furaha spend her five hundred shilings? (She used it to buy two pencils and an eraser)	$3\frac{1}{2}$	0
<b>Total</b>			



*Kiambatisho Na. 5: Karatasi ya Upimaji Stadi ya Kuandika*

*Jina la Mwanafunzi \_\_\_\_\_*

*Namba ya Mwanafunzi \_\_\_\_\_*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
UPIMAJI WA DARASA LA PILI  
202 STADI YA KUANDIKA**

*Muda: Dakika 40 Alhamisi, 11 Aprili 2019 asubuhi*





---







*Maelekezo*

- 1. Karatasi hii ina maswali matatu (3).*
- 2. Jibu maswali yote.*
- 3. Andika majibu yako yote kwa kutumia penseli.*
- 4. Andika jina lako na namba yako katika kila ukurasa.*

<i>KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU</i>		
<i>Namba ya Swali</i>	<i>Alama</i>	<i>Saini ya Mpimaji</i>
<i>1.</i>		
<i>2.</i>		
<i>3.</i>		
<i>Jumla</i>		

1. Tazama kwa makini picha zifuatazo kisha andika majina yake katika nafasi zilizo wazi.

<p>(a)</p>	 <hr/>	<p>(b)</p>	 <hr/>
<p>(c)</p>	 <hr/>	<p>(d)</p>	 <hr/>

<p>(e)</p>	 <hr/>	<p>(f)</p>	 <hr/>
<p>(g)</p>	 <hr/>	<p>(h)</p>	 <hr/>
<p>(i)</p>	 <hr/>	<p>(j)</p>	 <hr/>

2. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa.

(a) MKATE, chungwa, mlima, KIJIKO

(b) BLUU, kijani, NYEKUNDU, manjano

(c) SAA, mkuki, CHAKI, karatasi

(d) Paka, SIMBA, pundamilia, NYANI

(e) SHATI, sketi, GAUNI, suruali

3. Nakili kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: nukta (·), mkato (,), alama ya kushangaa (!), na alama ya kuuliza (?) mahali panapostahili.

Jamani eeh\_\_ Basi la kwenda nyumbani kwetu limetuacha\_\_ Sasa je\_\_ tutaondoka na usafiri wa basi gani\_\_

---

---

---

---

Pupil's Name \_\_\_\_\_

Pupil's Number \_\_\_\_\_

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA  
STANDARD TWO ASSESSMENT

202

WRITING SKILLS







Time: 40 Minutes Thursday, 17<sup>th</sup> April 2019 morning





*Instructions*

1. This paper has three (3) questions.
2. Answer all questions.
3. Write all your answers in pencil.
4. Write your name and number on every page.

<i>FOR ASSESSOR'S USE ONLY</i>		
<i>Question Number</i>	<i>Marks</i>	<i>Assessor's Signature</i>
1.		
2.		
3.		
<i>Total</i>		

7. Study the pictures below carefully and then write their names in the spaces provided.

<p>(a)</p>	 <hr/>	<p>(b)</p>	 <hr/>
<p>(c)</p>	 <hr/>	<p>(d)</p>	 <hr/>
<p>(e)</p>	 <hr/>	<p>(f)</p>	 <hr/>

(g)	 <hr data-bbox="299 548 644 556"/>	(h)	 <hr data-bbox="864 548 1251 556"/>
(i)	 <hr data-bbox="386 973 675 981"/> <hr data-bbox="299 1051 644 1058"/>	(j)	 <hr data-bbox="864 1051 1232 1058"/>

2. Underline the words which are written in capital letters.

(i) BREAD, orange, mountain, SPOON

(ii) BLUE, green, RED, yellow

(iii) WATCH, spear, CHALK, paper

(iv) Cat, LION, zebra, MONKEY

(v) SHIRT, skirt, DRESS, trousers

3. Copy the following paragraph in the space given and then put the punctuation marks: full stop (.), comma (,) exclamation mark (!) and question mark (?) where necessary.

My goodness \_\_ The bus has already left \_\_ So  
\_\_ which bus are we going to travel by \_\_

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
UPIMAJI WA DARASA LA PILI  
203 STADI YA KUHESABU

Muda: Saa 1 Alhamisi, 11 Aprili 2019 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina maswali ishirini (20).
2. Jibu maswali yote.
3. Andika majibu yote kwa penseli.
4. Andika namba na jina lako katika kila ukurasa.

KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU

Namba ya Swali	Alama	Saini ya Mpimaji	Namba ya Swali	Alama	Saini ya Mpimaji	Namba ya Swali	Alama	Saini ya Mpimaji	Namba ya Swali	Alama	Saini ya Mpimaji
1.			7.			13.			19.		
2.			8.			14.			20.		
3.			9.			15.					
4.			10.			16.					
5.			11.			17.					
6.			12.			18.					

*Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi.*

1. 4, 5, \_\_, 7, 8, 9.
2. 15, \_\_, 13, 12, 11.
3. 44, 46, \_\_, 50, 52.
4. 70, 80, 90, \_\_.
5. 25, 30, \_\_, 40, 45.

*Tafuta Majibu:*

6.  $1 + 7 = \underline{\quad}$
7.  $12 + 5 = \underline{\quad}$
8.  $28 + 6 = \underline{\quad}$
9.  $47 + 16 = \underline{\quad}$
10. *Shilingi 400 + shilingi 50 =  $\underline{\hspace{2cm}}$*
11.  $8 - 5 = \underline{\quad}$
12.  $19 - 4 = \underline{\quad}$
13.  $25 - 7 = \underline{\quad}$
14.  $67 - 18 = \underline{\quad}$

15. Shilingi 700 - shilingi 550 = \_\_\_\_\_

16. Mary ana machungwa 240 na kaka yake ana machungwa 342. Je, jumla wana machungwa mangapi?

---

---

---

---

17. Sara alikuwa na pipi 450. Alimgawia rafiki yake pipi 220. Je, alibakiwa na pipi ngapi?

---

---

---

---

18. Darasa la pili lina wasichana 70 na wavulana 90. Je, darasa hilo lina wanafunzi wangapi?

---

---

---

---

19. Juma alinunua kalamu kwa shilingi 150 na daftari kwa shilingi 500. Je, alilipa shilingi ngapi?

---

---

---

---

---

20. Musa alipewa shilingi 600 na baba yake. Alitumia shilingi 250. Je, alibakiwa na shilingi ngapi?

---

---

---

---

---

---

Jina la Mwanafunzi \_\_\_\_\_

Namba ya Mwanafunzi \_\_\_\_\_

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA  
STANDARD TWO ASSESSMENT  
203 ARITHMETIC SKILLS

Time: 1 Hour

Thursday, 11<sup>th</sup> April 2019 morning

*Instructions*

1. This paper has twenty (20) questions.
2. Answer all questions.
3. Write your answers in pencil.
4. Write your name and your number on each page.

FOR ASSESSOR'S USE ONLY											
Question Number	Score	Assessor's Initials	Question Number	Score	Assessor's Initials	Question Number	Score	Assessor's Initials	Question Number	Score	Assessor's Initials
1.			7.			13.			19.		
2.			8.			14.			20.		
3.			9.			15.					
4.			10.			16.					
5.			11.			17.					
6.			12.			18.					

*Write the missing number:*

1. 4, 5, \_\_, 7, 8, 9.

2. 15, \_\_, 13, 12, 11.

3. 44, 46, \_\_, 50, 52.

4. 70, 80, 90, \_\_.

5. 25, 30, \_\_, 40, 45.

*Work out the answers:*

6.  $1 + 7 = \underline{\hspace{2cm}}$

7.  $12 + 5 = \underline{\hspace{2cm}}$

8.  $28 + 6 = \underline{\hspace{2cm}}$

9.  $47 + 16 = \underline{\hspace{2cm}}$

10.  $400 \text{ shillings} + 50 \text{ shillings} = \underline{\hspace{4cm}}$

11.  $8 - 5 = \underline{\hspace{2cm}}$

12.  $19 - 4 = \underline{\hspace{2cm}}$

13.  $25 - 7 = \underline{\hspace{2cm}}$

14.  $67 - 18 = \underline{\hspace{2cm}}$

15.  $700 \text{ shillings} - 550 \text{ shillings} = \underline{\hspace{2cm}}$

16. *Mary has 240 oranges and her brother has 342 oranges. How many oranges do they have altogether?*

---

---

---

---

17. *Sara had 450 sweets. She gave her friend 220 sweets. How many sweets was she left with?*

---

---

---

18. *A standard two class has 70 girls and 90 boys.  
How many pupils are in the class?*

---

---

---

---

---

---

---

19. *Juma bought a pen for 150 shillings and an  
exercise book for 500 shillings. How much did  
he pay?*

---

---

---

---

---

---

---

20. *Musa was given 600 shillings by his father. He  
spent 250 shillings. How much money was he  
left with?*



---

---

---

---

---

---

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHE SABU**

**DODOSO LA MWALIMU MKUU WA SHULE**

**Jina:** \_\_\_\_\_

**Shule Unayoongoza:** \_\_\_\_\_

**1. Taarifa za shule kwa ujumla**

*Tafadhali jaza taarifa kuhusu wanafunzi na walimu wa KKK katika shule yako kwa kuandika katika visanduku ulivyopewa.*

- (i) Kuna wanafunzi wangapi waliodahiliwa katika darasa la I na la II waliopo shuleni kwa sasa?
- (ii) Walimu wangapi wanafundisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu darasa la I na la II katika shule yako?
- (iii) Kati ya walimu wanaofundisha stadi za KKK, Walimu wangapi wana mafunzo maalumu ya kufundisha stadi hizo?
- (iv) Je shule ina mikondo mingapi ya wanafunzi wa darasa la I?
- (v) Mikondo ya wanafunzi wa darasa la I uliyoitaja katika (iv) hapo juu ina wanafunzi wangapi kila mmoja (jaza wastani kama idadi hailingani)
- (vi) Je shule ina mikondo mingapi wa wanafunzi wa darasa la II?
- (vii) Mikondo ya wanafunzi wa darasa la II uliyoitaja katika (iv) hapo juu ina wanafunzi wangapi kila mmoja (jaza wastani kama idadi hailingani)

Je shule ina Muhtasari wa Kufundishia stadi za KKK kwa darasa la Kwanza na la Pili? Ndiyo  Hapana

## 2. Taarifa kuhusu Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia.

*Tafadhali jaza maoni yako kuhusu uwepo wa vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia kwa kuzungushia namba ya uchaguzi unaolingana na maoni yako kuhusu vifaa hivyo hapo shuleni kwako.*

NA	Swali	Hafifu (2)	Chini ya Wastani (2)	Wastani (3)	Mzuri (4)	Mzuri Sana (5)
(i)	Upatikanaji wa Vitabu vya kiada vya kufundisha stadi za Kuhesabu unaweza kuelezewa kuwa ni:	1	2	3	4	5
(ii)	Upatikanaji wa vitabu vya ziada vya mazoezi ya stadi ya kuhesabu unaweza kuelezewa kuwa ni:	1	2	3	4	5
(iii)	Uwepo wa Vifaa vya kufundishia stadi ya kuhesabu (kama vile vihesabio na vifaa vingine) unaweza kuelezewa kuwa ni;	1	2	3	4	5
(iv)	Uwepo wa Vifaa vya kufundishia stadi ya Kuandika (kama vile vibao na vifaa vingine) unaweza kuelezewa kuwa ni;	1	2	3	4	5
(v)	Je uwepo wa vitabu vya kiada vya kufundishia stadi ya kusoma unaweza kuelezewaje?	1	2	3	4	5
(vi)	Je unaweza kuelezeaje upatikanaji wa vifaa					

<b>NA</b>	<b>Swali</b>	<b>Hafifu (2)</b>	<b>Chini ya Wastani (2)</b>	<b>Wastani (3)</b>	<b>Mzuri (4)</b>	<b>Mzuri Sana (5)</b>
	vianvyolenga kuendeleza stadi ya kusoma kama vile vitabu vya hadithi fupifupi kwa watoto wadogo?	1	2	3	4	5

### **3. Taarifa kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji**

*Tafadhali jibu maswali kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzungushia namba inayolingana na maoni yako kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK katika shule yako.*

<b>NA</b>	<b>Swali</b>	<b>Hafifu (2)</b>	<b>Chini ya Wastani (2)</b>	<b>Wastani (3)</b>	<b>Mzuri (4)</b>	<b>Mzuri Sana (5)</b>
(i)	Uwepo wa madawati, viti na meza za kukalia watoto na walimu shuleni kwako wakati wa kujifunza unaweza kuelezewa kuwa ni:	1	2	3	4	5
(ii)	Ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wa darasa la I na la II waliopo shuleni kwa sasa, hali ya uwepo wa vyumba vya madarsa inaweza kuelezewa kuwa ni:	1	2	3	4	5
(iii)	Je mazingira ya upatikanaji wa chumba maalumu au makataba ambapo watoto na walimu wanaweza kuazima vitabu ili kuwawezesha	1	2	3	4	5

NA	Swali	Hafifu (2)	Chini ya Wastani (2)	Wastani (3)	Mzuri (4)	Mzuri Sana (5)
	wanafunzi kujifunza zaidi stadi za KKK hata baada ya muda wa shule yakoje?					

**4. Taarifa nyinginezo**

Je ni jambo gani ambalo halikuulizwa kwenye dodoso hili kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ambalo ungependa Baraza la Mitihani lifahamu? (Toa maelezo mafupi)

---



---



---

**5. Changamoto zinazojitokeza wakati wa ujifunzaji wa wanafunzi wa stadi za KKK kuwa mgumu**

*Tafadhali jibu maswali kuhusu changamoto zinazojitokeza ambazo zinafanya ujifunzaji wa wanafunzi wa stadi za KKK kuwa mgumu kwa kuzungushia namba ya changamoto inayojitokeza zaidi. (unaweza kuzungushia changamoto zaidi ya moja)*

- (i) Umbali wa wanafunzi wengi kutoka shule ilipo
- (ii) Wanafunzi kukosa masomo mara kwa mara kutokana na mahudhurio yasiyoridhisha
- (iii) Uhaba wa walimu ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi
- (iv) Kupokea wanafunzi wanaohamia ambao stadi zao za KKK haziridhishi.
- (v) Uhaba wa vitendea kazi kama vile vitabu ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi.
- (vi) Changamoto nyinginezo (Zitaje)

---



---



---

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU 2018**

**DODOSO LA MWALIMU (MSIMAMIZI)**

**Jina:** \_\_\_\_\_ **Mkoa** \_\_\_\_\_

**Halmshauri** \_\_\_\_\_ **Shule :** \_\_\_\_\_

**Mkondo Uliosimamia:** \_\_\_\_\_ **Namba ya Simu:** \_\_\_\_\_

1. Je, umesimamia idadi ya wanafunzi wangapi katika stadi ya :

(i) Kuandika

(ii) Kuhesabu

(iii) Kusoma

2. Je wakati wa kusimamia vifaa vyote vilivyohitajika katika kufanya upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu vilitosheleza?

Ndiyo

Hapana

(a) Kama jibu ni hapana taja aina ya vifaa ambavyo havikutosheleza. \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

(b) Taja hatua zilizochukuliwa kutatua upungufu huo.  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

3. Je, kuna wanafunzi walioshindwa kufanya upimaji? Kama

wapo waorodheshe majina yao na sababu za kushindwa kufanya upimaji.

<b>Na</b>	<b>Jina</b>	<b>Sababu za Kushindwa Kufanya Upimaji</b>
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		

4. Umewahi kupokea kitabu chenye taarifa ya uchambuzi wa upimaji wa KKK wa mwaka 2017 na kukitumia?.

Ndiyo  Hapana

5. (a) Unafikiri vitabu hivyo vina tija katika kuborehsha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK?

Ndiyo  Hapana

- (b) Toa maelezo mafupi kwa jibu lako hapo juu.

---

---

---

---

**Asante kwa ushirikiano**

